# Nipashe

Ijumaa Mei 24, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579926

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Sethi alia na Magereza kumzuia kumwona wakili

UKURASA 3




# Ndugai: Masele usitufitinishe



• **Amtaka** aache kumchonganisha na JPM, Bunge lamsamehe kufungiwa, mwenyewe afunguka... *Ukurasa 2*

## Semina ilivyotafuna bil. 1.1/- Ngorongoro

UKURASA 2

## Madini yaingiza mil. 300/- siku 20



UKURASA 21



Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, akizungumza bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

**MICHEZO** **ZAHERA AMPA AJIBU 'NONDO'** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Ndugai: Masele acha fitina

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

HATIMAYE sakata la tuhuma za utovu wa nidhamu zilizokuwa zinamkabili Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele (CCM), limehitimishwa bungeni baada ya Spika Job Ndugai kuwaomba wabunge wampuuze na kumsamehe.

Hata hivyo, Spika Ndugai alimtaka Masele, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), kuacha kupeleka maneno ya fitina na uchonganishi kwa Rais John Magufuli kwa kuwa kiongozi huyo wa nchi ana mambo mengi ya kulitumikia taifa.

Jumatatu, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilimhoji Masele kutokana na agizo la Spika Ndugai kumtaka kufika mbele ya kamati hiyo kujibu tuhuma za kughushi nyaraka, kutohudhuria vikao vya Bunge bila kibali cha Spika, kudharau wito wa kurejea nchini kuhojiwa na kuchonganisha mihimili ya nchi.

Baada ya Kamati ya Maadili kuwasilisha bungeni shauri hilo, ikimtia hatiani Masele na kupendekeza Bunge liazimie kumfungia kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo kuanzia jana, lakini Spika Ndugai aliwataka wabunge wamsamehe huku akisisitiza aache uongo na fitina.

"Jambo hili ni la kipekee katika bunge letu, ndiyo maana nikasema ni vizuri tuwe na utulivu mkubwa na usikilizaji mkubwa, naomba tusikilizane. Kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Masele haelewi hata hivi sasa ni nini kinachoendelea.

"Masele hakuitwa nyumbani kwa sababu ya jambo lolote la huko (PAP), tungemwitaje kwa jambo la PAP? Mambo yanafanyika huko wanaopaswa kutuarifu kinachofanyika huko ni hawa wabunge wawakilishi wetu.

"Sasa tungemwitaje nyumbani kwa mambo ya huko? Tumemwita nyumbani na nimerudia tena na tena na kila nikirudia, anapotosha migogoro ambayo sisi hatuko nayo," alisema.

Spika alilieleza Bunge kuwa Masele aliziandikia mamlaka za juu ujumbe wa uchonganishi, akigonganisha Bunge na serikali na ndiyo sababu ya kumtaka arejee nchini kutoka Afrika Kusini ili ahojiwe kuhusu tuhuma hizo.

"Tukapeleka barua sehemu tatu, ilienda ubalozi wa kwetu

INAENDELEA UK. 8

# Kijana afukua kaburi la babaye

**Na Romana Mallya**

UKISIKIA dunia imekwisha ni pamoja na tukio la kijana Joseph Saluni (28), mkazi wa kijiji cha Mwakwaru Ngalitati Wilaya ya Siha, Moshi mkoani Kilimanjaro, ambaye amefukua kaburi la baba yake.

Kijana huyo anadaiwa kufukua kaburi la mzazi wake huyo aliyefariki dunia miaka mitatu iliyopita na kuchukua blanketi ili kujisitiri na baridi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Hamisi Issah, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo huko wilayani Siha.

Kamanda Issah alisema Saluni aliamua kufukua kaburi hilo la baba yake bila kibali ili kuchukua blanketi ambalo mwili wa baba yake ulifunikwa.

"Huyu kijana amefukua kaburi la baba yake aliyezikwa miaka mitatu iliyopita na kisa cha kufukua alidai kwamba kutokana na hali ya hewa anahitaji blanketi alilozikiwa baba yake na bila ajizi alikwenda kufukua kaburi," alisema.



Magari yakipita kwa tabu kutokana na mafuriko ya maji katika sehemu ya Barabara ya Nkrumah, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: JOHN BADI**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
23/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 29/05/2019 kampuni ya SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA)LTD itasafirisha mizigo yake yenye vipimo vikubwa Kutoka SUMBAWANGA kuelekea KAMBANGA kupitia MPANDA , Magarii yenye namba za usajili:
   1. **T349 BNT/T646 BCJ**
   2. **T550 BES/T474BCJ**
   3. **T389 BES/T668 BCJ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 20.00**
   **Upana** - **mita 2.99**
   **Kimo** - **mita 5.1**
3. Njia itakayotumika **SUMBAWANGA hadi KAMBANGA** kupitia MPANDA.gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115245202


# Semina zilivyotafuna bil. 1.1/- Ngorongoro

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imeitaka serikali kuchukua hatua kuhusu matumizi mabaya ya fedha katika Mamlaka ya Bonde la Ngorongoro.

Akiwasilisha maoni ya kambi hiyo kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka ujao wa fedha kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika wizara hiyo, Mch. Peter Msigwa, Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Ruge (Chadema), alisema wamebaini matumizi mabaya ya fedha katika mamlaka hiyo kupitia semina na vikao.

Alisema bodi ya mamlaka hiyo ilifanya jumla ya vikao 20 na semina sita kwa mwaka wa fedha 2017/18 na kutumia Sh. bilioni 1.1 (Sh. 1,102,907,602).

Ruge alibainisha kuwa fedha hizo zilitumika kwa posho za kujikimu Sh. milioni 799.906, fedha kwa ajili ya mafuta Sh. milioni 81.226, gharama za ukumbi Sh. milioni 29.321, chakula na viburudisho Sh. milioni 34.449, malazi Sh. milioni 57.459 na gharama nyingine za usafiri Sh. milioni 100.545.

"Matumizi ya namna hii ya kuwakirimu wajumbe wa bodi, yanaweza kuleta tafsiri kuwa lengo la menejimenti ni kuwaghiribu wajumbe wa bodi ili ishindwe kufanya au kutekeleza jukumu lake la msingi la kuisimamia menejimenti hiyo.

"Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona litakuwa ni jambo la busara waziri kuielekeza Bodi ya Bonde la Ngorongoro kujitathmini na kuona kama bado inao uhalali wa kuendelea kuisimamia menejimenti," alisema.

Ruge pia alisema biashara ya uwindaji imekuwa na changamoto zinazokatisha tamaa wawekezaji. Alisema ni biashara inayoelemewa na wingi wa kodi, akibainisha kuwa katika sekta ndogo ya uwindaji, kuna takribani tozo 21 za kodi kubwa kuachilia mbali zile za biashara ya utalii.

Kambi hiyo pia ilitahadharisha serikali kuwa bila kulinda demokrasia, nchi itaanguka kiutalii kama ilivyotokea kwa Sri Lanka ambayo utalii wake umeporomoka kwa asilimia 43 ndani ya mwaka mmoja kutokana na misukosuko ya kisiasa.

Kwa upande wake, Makamu

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Sethi alilia mahakama kumwona wakili wake

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Habinder Sethi anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, kumpa kibali cha kuonana na wakili wake mahabusu ya gereza la Ukonga kwa sababu miezi sita sasa imepita bila kuwasiliana naye.

Seth na mwezake James Rugemarila, walifikishwa kwa mara ya kwanza katika mahakama hiyo Juni 19, 2017, wakikabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, hivyo kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh 309,461,300,158.27

Bilionea huyo alitoa madai yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi wakati kesi hiyo ilipotajwa.

Awali, Wakili wa Serikali Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi bado haujakamilika.

Hata hivyo, Sethi aliomba mahakama imruhusu kutoa malalamiko yake na hatiaye ilimkubalia.

"Mheshimiwa hakimu, wakili wangu anapokuja gerezani kupata maelekezo yangu, maofisa wa gereza wanamzuia. Naiomba mahakama hii imruhusu wakili wangu aje nizungumze naye kuhusu mustakabali wa kesi yangu. Nina miezi sita sasa sijapata haki yangu ya kisheria," alidai Sethi.

Kutokana na madai hayo, Hakimu Shaidi aliwaagiza maofisa wa magereza wamruhusu wakili wake ili aonane na mshtakiwa huyo kwa kuwa ni haki yake ya msingi kuonana naye.

Alisema kesi hiyo itatajwa Juni 10, mwaka huu, itakapokuja kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa warudishwe rumande.

Sethi na Rugemarila wanakabiliwa na mashtaka 12 ya uhujumu uchumi kwa kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi, kutoa nyaraka za kughushi.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa wanadaiwa kuwa kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la pili la kujihusisha na mtandao, washtakiwa hao kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19,2014 jijini Dar es Salaam wakiwa si watumishi wa umma wanadaiwa kutekeleza mtandao huo wa uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Katika shtaka la tatu, Sethi anadaiwa kuwa Oktoba 10, 2011 katika mtaa wa Ohio Ilala jijini Dar es Salaam. akiwa na nia ya ulaghai, alighushi fomu namba 14 ya usajili wa kampuni na kuonesha yeye ni Mtanzania anayeishi Kitalu namba 887 Mtaa wa Mrikau, Masaki wakati akijua ni uongo.

# Moto wateketeza mali za wanafunzi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira iliyopo Marangu katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro wamenusurika kifo, huku zaidi ya 73 wakipoteza vifaa vyao vyote, baada ya mabweni mawili kuteketea kwa moto.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, amethibitisha kuwa licha ya samani na vifaa mbalimbali kuteketea, hakuna madhara yaliyojitokeza kwa binadamu.

Kwa mujibu wa Warioba, moto huo uligundulika saa 2:09 asubuhi wakati wanafunzi wakiwa darasani.

Alisema mabweni yaliyoteketea kwa moto ni Muungano ambalo linachukua wanafunzi 244 na hakuna kitu kilichookolewa.

Wanafunzi wamepoteza vifaa vyao yakiwamo magodoro, madaftari na nguo zao.

"Bweni jingine lililoungua ni la Japan ambalo linabeba wanafunzi 53 ambalo limeteketea lote na vifaa vyote," alisema.

Kwa mujibu wa Warioba, hadi sasa vikosi vya Polisi, Zimamoto na Uokoaji na taasisi nyingine hawajagundua chanzo cha tatizo hilo.

"Tunaendele na uchunguzi wa nini chanzo cha moto kwani imebainika kubwa na mabweni hayo hayana vyanzo vya umeme vya pamoja," alisema Warioba.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuwa watulivu na kusaidiana hasa wanapomuona mwenzao ana tatizo wakati halmashauri ikitafuta namna ya kupata vifaa ili kurejea katika hali yao ya kawaida.

"Sisi kama serikali tupo tayari kuimarisha ulinzi na usalama wenu, hivyo jitahidini kurudi katika hali yenu ya kawaida kwa kuwa hakuna lolote litakalowadhuru na serikali hii ni makini ndio maana tupo hapa leo na tutahakikisha leo mnapata sehemu ya kulala," alisema.

Mkuu wa Shule hiyo Elizabeth Abdallah, alisema wamefanya jitihada katika kuhakikisha wanafunzi wote wapo salama.

Alisema wanafunzi waliobaki shuleni ni wa kidato cha tano zaidi ya 331 ambapo wa kidato cha sita wameshaondoka baada ya kumaliza mitiani yao ya kidato cha sita mwaka huu.

Mwanafunzi wa kidato cha tano, Mwanamkasi Abdallah, aliiomba serikali kuhakikisha inaongeza usalama kwa wanafunzi na kuchunguza chanzo cha moto huo na kudhibiti ipasavyo.


ELCT – NORTH CENTRAL DIOCESE
SELIAN LUTHERAN HOSPITAL
P.O. BOX 3164 ARUSHA TANZANIA
E – mail: selianlh@habari.co.tz

## INVITATION FOR EXPRESSION OF INTEREST

Selian Lutheran Hospital in Ngaramtoni – Arusha is inviting applications for prequalification and registration of suppliers. We seek to establish framework agreements for a period of one year as per the categories of goods and services listed below:-

| Reference No. | | Item Description |
|---|---|---|
| SLH/ EOI /2019/001 | - | Stationery for office supplies |
| SLH/ EOI /2019/002 | - | Printing services |
| SLH/ EOI /2019/003 | - | Detergents, Antiseptic |
| SLH/ EOI /2019/004 | - | Medicine, Medical Supplies & Medical Equipment |
| SLH/ EOI /2019/005 | - | Motor vehicle service and maintenance |
| SLH/ EOI /2019/006 | - | Laboratory reagents & Equipment |
| SLH/ EOI /2019/007 | - | Motor vehicle & Property Insurance |
| SLH/ EOI /2019/008 | - | Maintenance of fire extinguishers/Fire equipment |
| SLH/ EOI /2019/009 | - | Fumigation services |
| SLH/ EOI /2019/010 | - | Canteen and catering services |
| SLH/ EOI /2019/011 | - | Electrical materials & Plumbing Material |
| SLH/ EOI /2019/012 | - | Fuel and Lubricants (Diesel) |
| SLH/ EOI /2019/013 | - | Oxygen (O2) Carbon Dioxide(CO) and Nitrous Oxide (NO) gas |
| SLH/ EOI/2019/014 | - | Auditing Services |

If your company is interested in undertaking any of the services mentioned above please submit the documents and information listed below:-

a) Company profile
b) Business registration certificate /Certificate of incorporation /Business license
c) Tin Number
d) EFD Receipt (evidence of use of EFD Machine)
e) Provide the most recent price list

To reach Medical Director, Selian Lutheran Hospital, P.O. Box 3164 Arusha, not later than 14th June 2019, Time 15:00hrs.

All current suppliers are advised to re-apply. Selian Lutheran Hospital reserves the right to accept or reject any application or part thereof, and is not bound to give reason for its decision.

Tender document will be available at the Hospital Offices in Ngaramtoni with non refundable fee of Tsh.50, 000/=.

215245602



CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA
THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT
SHAABAN ROBERT STREET
P. O. BOX 3918
TEL: (+255) 22 2112931 - 4; 22 2114817
FAX: 22 2112935
rector@ifm.ac.tz
DAR ES SALAAM
TANZANIA

## TANGAZO

## VYETI KWA WAHITIMU WA MWAKA 2018

Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kinawatangazia wahitimu wa mwaka 2018 kuwa vyeti vyao vipo tayari. Orodha kamili ya vyeti vilivyopo tayari inapatikana kwenye tovuti ya chuo yaani www.ifm.ac.tz.

Vyeti vinatolewa kwenye ofisi ya kumbukumbu za wanafunzi na takwimu chumba namba D005, Block D {IFM Main Campus} na Mwanza Teaching Centre kila siku za wiki kuanzia saa 03.00 asubuhi mpaka 12.00 jioni na Jumamosi kuanzia saa 04.00 asubuhi mpaka saa 09.00 alasiri kwa kipindi cha mwezi mmoja tokea siku ya tangazo hili. Baada ya muda huu wa mwezi mmoja, vyeti vitatolewa kila siku kuanzia saa 08:00 mchana mpka saa 10:00 alasiri kila siku za kazi.

**UFIKE NA NYARAKA ZIFUATAZO**

1. Kitambulisho cha chuo,
2. Kopi ya 'Academic Transcript'ya kozi uliyomaliza.

***KWA WALIOPOTEZA KITAMBULISHO CHA CHUO UFIKE NA RIPOTI YA POLISI PAMOJA NA KITAMBULISHO KINGINE CHENYE TAARIFA ZAKO SAHIHI.***

**IMETOLEWA NA OFISI YA MSAJILI; CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA**
**20TH MAY 2019.**

215245502

# Wambura mahabusu bado yamhusu

**Na Hellen Mwango**

MAKAMU wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, ataendelea kukaa mahabusu baada ya kesi yake kuahirishwa kwa mara nyingine hadi Juni 4, mwaka huu.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha iliahirishwa baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Juni 4, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, kigogo huyo wa mpira wa miguu anakabiliwa na mashtaka 17, yakiwamo ya kughushi, kutoa na kuwasilisha nyaraka za uongo, mashtaka 13 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu

INAENDELEA UK. 8



Kiongozi wa Jukwaa la Tafakuri na Mkurugenzi Mtendaji wa Uhuru Media Group, Ernest Sungura, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Jukwaa la Pili la Tafakuri litakalofanyika Siku ya Afrika, Mei 25 mwaka huu, katika ukumbi wa Nkrumah wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Uhuru, Josephat Mwanzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Tozo zaidi zenye kero kufutwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeanza jitihada za kufuta tozo zote ambazo zinakwamisha mazingira ya ufanyaji wa biashara zikiwamo za kwenye pembejeo.

Hatua ya kufuta tozo hizo ili kuwawezesha wafanyabiashara kuzifikisha hadi ngazi ya kijiji kwa wakulima.

Majaliwa alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Madaba, Kizito Mhagama, katika kipindi cha 'Maswali ya papo hapo kwa Waziri Mkuu'. Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kupunguza tozo kwa maduka yanayouza pembejeo ili kumwezesha mkulima kupata pembejeo.

Waziri Mkuu alisema serikali imepokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara mbalimbali wakiwamo wauzaji wa pembejeo juu ya tozo mbalimbali katika uendeshaji wa shughuli zao za biashara.

"Serikali imesikia vilio vyao na sasa inafanya mapitio ya tozo hizo na itakapofikia hatua nzuri itawajulisha na kuwashirikisha kujua ni aina gani ya tozo ambayo itaondolewa au kuibadilisha ili waendelee kufanya biashara zao katika mazingira rahisi," alisema.

Kwa mujibu wa Majaliwa, kazi kubwa inayofanywa na serikali kwa sasa ni kufanya mapitio ya tozo zote kuanzia kwa wakulima hadi kwa wafanyabiashara na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara nchini, ikiwamo ya pembejeo ili kuzifikisha kiurahisi kwa wakulima.

Hata hivyo, Waziri Mkuu alisema kwamba tayari mawaziri wa kisekta wenye dhamana ambao wana tozo mbalimbali kwenye wizara zao zinazokwamisha ufanyaji biashara katika mazingira rafiki, wameshakutana kwa ajili ya kujadili namna ya kulipatia ufumbuzi suala hilo.

"Hata juzi nilikuwa na mawaziri hao kupata taarifa kwa pamoja kuona maeneo yote waliyoyapitia na tozo zote zinazokusudiwa kupitiwa upya na kazi hiyo ikikamilika watakutana na Kamati ya Bajeti ya Bunge, Wizara ya Fedha ili kuona namna nzuri ya kuondoa tozo hizo. Lakini baadaye suala hilo litaenda kwenye mamlaka inayotoa ridhaa ya kuondoa au kupunguza tozo," alisema.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu alisema miradi mingi ya maji ambayo inatekelezwa kwenye maeneo mbalimbali nchini baadhi yake haitekelezwi kwa viwango vilivyokusudiwa, hivyo haiwiani na thamani halisi ya kiasi cha fedha kinachotolewa.

Hata hivyo, Waziri wa Maji wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka 2019/20 alieleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa dhidi ya miradi yote ambayo haiwiani na kiasi cha fedha kilichotolewa pamoja na hatua zilizochukuliwa dhidi ya miradi yote.

Waziri Mkuu ameyaesema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Korogwe Mjini, Mary Chatanda (CCM), aliyetaka kujua serikali kama iko tayari kuchunguza na kuchukua hatua kwa watendaji walioshindwa kusimamia miradi ya maji na kuisababishia hasara pamoja na wananchi kukosa huduma waliyokusudiwa.




# Mwandishi Mkuu wa Sheria ateuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Onorius John Njole kuwa Mwandishi Mkuu wa Sheria (Chief Parliamentary Draftsman - CPD).

Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilieleza jana kuwa, uteuzi wa Njole ulianza jana.

Kabla ya uteuzi huo, Njole alikuwa Mkurugenzi wa Sheria na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

Iliongeza kuwa Njole anachukua nafasi ya Sara K. Barahomoka ambaye anastaafu.

## TANGAZO


game
7 DAYS ONLY
Deals valid 25 - 31 May 2019
View this catalogue online www.game.co.tz
We'll beat any price, so you get more with every shop.
Dare to Compare
Bakers Eet Sum Mor 200g
3500
Snickers Chocolate Bar 50g
1600
Kilombero Brown Sugar 1kg
2400
Azam Pure Wheat Flour 2kg
4500
Sunbelt Sunflower Oil Jelly Can 5l
28000
Africafe Instant Coffee 100g
6500
Nestle Milo Can 500g
13500
Royco Kora Mchuzi Mix 200g
2200
Weetabix Giant 900g
13000
Konyagi Gin 750ml
8000
Jack Daniels Whisky 750ml
56500
Safari Lager 500ml
2100
Minute Maid Apple 1.25l
2200
Kilimanjaro Natural Water 1.5l
850
Red Bull Energy Drink - 250ml
2600
Excessive alcohol consumption is harmful to your health, do not drive or operate machinery
Alcohol Not for Sale to Persons Under the Age of 18.
Dettol Soap Original 175g
2400
Colgate Maxfresh Spicy Fresh 100ml
2800
Maq Dish Washing Liquid 750ml
5150
Omo Hand Washing Powder 1kg
5500
Game is committed to offer you the best service with the lowest price. In the unlikely event that you find the same product advertised by a competitor at a lower price, we guarantee to beat that price! . T's & C's apply.
TANZANIA, DAR ES SALAAM
SHOPPING HOURS
View this catalogue online at www.game.co.tz ITEMS AVAILABLE WHILE STOCKS LAST
ALL PRICES LISTED ARE IN TANZANIAN SHILLINGS . ALL PRICES INCLUDE VAT.
Walmart
13800 | TANZANIA
215232102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dhuluma dhidi wakulima pamba haikubaliki kamwe

**WAKULIMA** kuendelea kukosa masoko ya uhakika ya mazao yao kutokana na vitendo vya ulanguzi wa bei unaofanywa na baadhi ya makampuni, ni kikwazo kwao na kinapaswa kupatiwa ufumbuzi. Watu binafsi na kampuni wanaojihusisha na ununuzi wa mazao ya wakulima wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa matatizo dhidi ya wakulima wetu, kutokana na kuwalipa bei ndogo ya mazao yao.

Hali hiyo inaonyesha kuwa baadhi ya watu binafsi na kampuni hawana lengo zuri la kufanyabiashara ya ununuzi wa mazao katika mfuko wa soko, bali ni kujali kupata faida kubwa bila kujali maslahi ya wakulima.

Hali hii imekuwa ikijitokeza wakati wa msimu wa ununuzi wa mazao ya biashara kama kahawa, chao, tumbaku, korosho na mengine mengi, kwa kuwalipa wakulima bei ndogo kinyume cha bei elekezi ambayo imekuwa ikitolewa na serikali.

Pamoja na serikali kujiondoa katika jukumu la kupanga bei ya mazao kama ilivyokuwa kabla ya Tanzania kuingia katika mfumo wa soko, ambao soko hujiendesha lenyewe, lakini watu wachache, wakiwamo wanunuzi wa mazao wamekuwa wakitumia vibaya fursa hiyo.

Bila kufanya hivyo, watu wachache wenye nia mbaya ya kujinufaisha zaidi wangewadhulumu wananchi katika hutuma na bei za bidhaa. Ndio maana serikali katika kutekeleza jukumu lake la kuweka mazingira bora na rafiki katika uendeshaji wa soko huria, iliamua kufuatilia kwa karibu ikiwamo kuweka bei elekezi katika bidhaa na huduma. Hata hivyo, tumeendelea kushuhudia baadhi ya wanunuzi wa mazao wakiendelea kutoa bei ndogo kwa wakulima kwa kutumia visingizio kadhaa kudanganya.

Kwa mfano, hivi sasa kuna malalamiko ya wakulima wa pamba wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, ambao wanalalamikia kupewa bei ndogo ya zao hilo baada ya msimu wa mauzo kuanza. Wanalalamikia walanguzi ambao wanawalipa Sh. 500 kwa kilo moja badala ya bei elekezi ya Serikali ya Sh. 1,200 kwa kilo moja.

Imeelezwa kuwa wakati Bodi ya Pamba ikiendelea na ukamilishaji wa upitishaji wa kampuni ambayo itakuwa ikinunua pamba kwa wakulima kupitia vyama vya msingi vya ushirika (Amcos), baadhi ya wafanyabiashara wameanza kutembea kwenye kaya za wakulima na kulangua pamba kwa Sh. 500 kwa kilo.

Mkaguzi wa pamba wilayani Kishapu, Thomas Tiluhongelwa, ambaye pia ni mwakilisha wa Bodi ya Pamba, alisema amesikitishwa na kitendo cha wakulima kulanguliwa pamba yao, huku akiwaonya wakulima hao kutokubali kulanguliwa pamba yao.


Akitoa onyo kali kwa wafanyabiashara wanaolangua pamba kwa wakulima, alisema watakaokwenda kinyume cha taratibu za Serikali kuwataka wanunuzi kuwalipa wakulima 1,200, pamba yake itataifishwa.

Kuendelea kuwalangua wakulima ni kuwaingiza kwenye umaskini, hivyo changamoto hiyo inapaswa kutafutiwa dawa ya kudumu ili wakulima wetu wanufaike na kilimo cha mazao yao. Mambo yaliyojitokeza katika msimu huu wa korosho yanapaswa kuipa serikali fundisho kwamba, kuna umuhimu wa kutafuta masoko yenye uhakika kwa ajili ya mazao ya wakulima.


Aidha, kuna haja ya kuyafuatilia kwa undani kampuni zinazokuja kununua mazao ya wakulima kabla ya kuyapatia leseni ikiwa kujiridhisha na historia yao, uwezo wa kifedha na uadilifu.

Kwa kufanya hivyo, wababaishaji hawatapata mwanya wa kujipenyeza kununua mazao na kusababisha matatizo kwa wakulima wetu. Kamwe tusikubali dhuluma dhidi ya wakulima wetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni wakati muafaka madalali vyama vya msingi kujitafakari

Na Yasmine Protace

**WIKI** hii tumeona na kusikia kupitia vyombo vya habari, vikinena mengi, kuhusu kuongezeka bajeti katika Wizara ya Kilimo.

Ongezeko hilo ni kutoka Sh. bilioni 170.2 hadi Sh. bilioni 253.85, ni neema kubwa katika sekta hiyo ya kilimo.

Hapana shaka, ni kiashiria kwamba sekta hiyo inafanya vizuri na iko katika sehemu ya wachangiaji mafanikio ya kuongezeka pato la taifa, huku ikimuwezesha mkulima kunufaika kimapato kupitia sekta yake.

Inakuwa jambo jema lenye kutoa kila sababu ya wakulima kunufaika na kile walichokilima, ili kiwaletee maendeleo.

Nianze kwa kuzungumzia uhalisia kwamba, hivi sasa mazao mengi yanapaswa kupelekwa sokoni kuuzwa na kumnufaisha moja kwa moja, tumekuwa tukimuona mkulima, ili aweze kuuza bidhaa zake, lazima dalali au vyama vya msingi kusimamia soko, ili mkulima afanye biashara.

Hata hivyo, kuna baadhi ya madalali na vyama vya ushirika, wamekuwa sio waaminifu na kusababisha wakulima kutonufaika na kupitia mazao ya wakulima hao.

Katika siku za karibuni katika semina ya Jinsia na Maendeleo zinazoandaliwa na asasi ya TGNP Mtandao. Baadhi ya washiriki walikuwa wakijadili mada inayozungumzia Bajeti katika Wizara ya Kilimo.

Katika semina hiyo, baadhi ya washiriki walichangia mada inayohusu Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya Mwaka 2018/2019 na mwaka 2019/2020.

Mjadala huo wa bajeti, uliibua mawazo tofauti ya washiriki, kutokana na kubaini fedha zinazotengwa katika Wizara ya kilimo. Baadhi ya washiriki walitoa maoni yao kupitia bajeti zinazotengwa.

Juliana Juma, anasema serikali inajitahidi kutoa pembejeo kwa wakulima, lengo ni kuwawezesha wakulima kupata mazao mengi, ili yawe mkombozi katika kuwainulia kipato.

Pamoja na serikali kutoa pembejeo wakulima kupata mazao mengi, changamoto inakuja katika upatikanaji masoko ya kuuza mazao hayo. Madalali wamekuwa wakiwatafuta wateja na kunufaika wao badala ya wakulima.

Mtoa maoni, Juma Amanzi, anasema madalali wanagawanyika katika makundi; waaminifu na wasio waaminifu. Pia, wapo wanaosimamia biashara za wakulima na wananufaika nazo, kwa namna wanazozijua.

Vivyo hivyo, kuna wanaojinufaisha kupitia mazao hayo ya wakulima, katika nyedo hizo za kidalali.

Ashura Juma, ana maoni kuwa, umefika wakati sasa wa wakulima kupewa elimu ya masoko, ili iwe mkombozi kwao kimapato.

Katika maoni yake, Ashura anasema kuwapo baadhi ya wakulima wanaolima matunda, lakini hawana masoko na kufanya matunda kuharibika kunayauiza. Kwani, iwapo wangekuwa na elimu ya usindikaji bidhaa hizo, zingeweza kuhifadhiwa kwa kipindi kirefu na kudumisha maufaa yake.

Hioyo ni sehemu ya hoja zilizoibuliwa na washiriki, katika semina, ombi ni kakapo sheria zitakazochukuliwa dhidi ya madalali, watakaoonekana kuhujumu mazao ya wakulima.

Mwingine mwenye maoni, Abdallah Hemed, anasema kuna vijiji ambavyo havina huduma za kibenki, lakini wakulima wake wanalima.

Hao ni kwamba, wanapopata matatizo, madalali hutumia matatizo hayo kuwapatia pesa kidogo, huku wakichukua mazao mengi kutoka kwa watu hao.

Nasema, kama mahali hapo kungekuwapo huduma za kibenki, wakulima wetu wangekuwa wanakopesheka. Lakini ndiyo hivyo, kutokuwapo huduma hizo, wanajikuta wakulima wakinyanyasika, huku mazao ni yao.

Huko vijijini, kinamama wanahangaika kulima, lakini wengi katika kundi hilo hawanufaiki na kilimo hicho. Kisa ni kwamba, wanahujumuwa kwa mazao yao kuanzia shambani hadi sokoni.

Niseme kinachotakiwa katika kuwanusuru kinamama wanufaike na kilimo chao, ni kwamba wawakilishi wao wawatafutie masoko ya uhakika, ikiwamo kuwachukulia hatua madali na vyama vya ushirika vyenye hujuma kwa mazao yao.

# Wasimamizi uchaguzi waapa, kujitoa rasmi vyama vya siasa

**Na Wandishi Wetu,**
DODOMA

WASIMAMIZI na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi mdogo wa udiwani unaotarajiwa kufanyika Juni 15, mwaka huu, wamekula kiapo cha kujitoa uanachama wa chama cha siasa mbele ya Hakimu Arnold Kirekiano.

Hatua hiyo imekuja baada ya Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Mbarouk Salum Mbarouk, kuwataka wasimamizi hao kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria zinazosimamia uchaguzi nchini.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika katika kata 32 nchini.

Jaji Mbarouk aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya usimamizi wa uchaguzi kwa wasimamizi na wasimamizi wasaidizi kutoka kata 32 na halmashauri 20 za Tanzania Bara zinazotarajia kushiriki katika uchaguzi huo, yanayofanyika jijini Dodoma.

Alisema pamoja na baadhi ya wasimamizi kuwa na uzoefu katika kusimamia uchaguzi mbalimbali, aliwasisitiza kuzingatia maelekezo watakayopewa na Tume kusimamia uchaguzi huo badala ya kufanya kwa mazoea kwa kuwa NEC imewaamini kuwa wanaweza kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Athumani Kihamia, aliwataka wasimamizi hao kuwapo muda wote wakati wa uchaguzi na hata pale inapotokea dharura wahakikishe anakuwapo msimamizi atakayetekeleza majukumu yao.

"Ni vyema mkafahamu kwamba kipindi hiki ambacho mmeshateuliwa na kuapa kuwa wasimamizi wa uchaguzi, wewe unakuwa mtumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa muda huo.

Kwa hiyo ni vyema ukawa ofisini muda wote ukiondoa dharura," alisema Dk. Kihamia.

Alifafanua kuwa suala hilo limetolewa mwongozo katika Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015 sehemu ya 4 (1), watendaji wote wa uchaguzi katika kipindi cha uteuzi wa wagombea, upigaji kura na hatua yoyote ya mchakato wa uchaguzi.



Mtuhumiwa wa biashara ya binadamu, Fatuma Saidi Ally (35), akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi katika Mahakama ya wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma jana, baada ya Mahakama hiyo, kumtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitatu jela. **PICHA: STEVIE CHINDIYE**

## UN kuadhimisha siku ya walinda amani leo

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa Mataifa (UN) leo unaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Walinzi wa Amani, huku ikiwahani askari sita kutoka Tanzania ambao walipoteza maisha kwenye shughuli za ulinzi wa amani kwenye nchi mbalimbali.

Itawakumbuka askari na walinzi wa amani 119 waliofariki wakiwa katika majukumu ya kulinda amani kuanzia mwaka 2018 hadi mwanzoni mwa mwaka huu.

Miongoni mwa askari watakaokumbukwa ni pamoja na Private Halum Hassan Nandala, Private Yulban Nziwa Nsevilwe, Koplo Erick Masauli John kutoka walinda amani wa UN katika Jamhuri ya Kati (Minusca), Private Mussa Shija Machibya, Koplo Mohammed Musa Omari na Private Mohammed Haji Alli ambaye alikuwa analinda amani katika Jeshi la UN Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (Monusco). Taarifa iliyotolewa jana na UN, ilieleza kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 12 zilizo mstari wa mbele katika kutoa askari wake kwenda kulinda amani katika nchi mbalimbali.

Ilieleza kuwa kwa taarifa za sasa, Tanzania imeshatoa askari zaidi ya 2,300 waliokwenda kulinda amani katika mji wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Lebanon na Sudan.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kaulimbiu kwa mwaka huu ni "Tuwalinde raia, Tulinde amani", ambapo Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, alisema kuwa kwa mwaka huu UN inatimiza miaka 20 tangu baraza la amani lilipoanzisha misheni ya kuwalinda raia.

Maadhimisho hayo nchini yatafanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam na yataongozwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi na UN.

# Majangili wabadili mwelekeo, wageukia kakakuona

**Na Salome Kitomari**

MAJANGILI wa wanyamapori wamebadili mwelekeo na sasa wanawinda kakakuona, ambaye magamba yake husafirishwa kwa ajili ya kutengenezea dawa mbalimbali ikiwamo kuongeza nguvu za kiume.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, mtaalamu wa usimamizi wa maliasili na sera wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Exper Pius, alisema hali hiyo imetokana na serikali kuimarisha sheria, sera, kanuni na kukabili mbinu za biashara ya meno ya tembo na pembe za ndovu.

Alisema biashara hiyo ndiyo inashika kasi duniani baada ya soko la meno ya tembo na pembe za ndovu kushuka thamani duniani, kutokana na nchi nyingi Tanzania ikiwamo kubana mianya ya biashara hiyo.

Pius alisema mwaka jana zaidi ya tani 14,000 za magamba ya kakakuona 36 kutoka Nigeria zilizokamatwa Singapore, na kwamba kasi ya biashara hiyo inazidi kuongezeka.

"Kwa Tanzania hakuna takwimu za idadi ya kakakuona au biashara hiyo kama ipo, lakini ni lazima kuchukua tahadhari kwa kuwa ndiyo biashara inayokuwa sana duniani kwa sasa baada ya kuwapo kwa udhibiti mkubwa wa biashara ya meno ya tembo na pembe za ndovu," alisema.

Alisema biashara hiyo imeshamiri kwenye nchi za Afrika Magharibi, na kwamba kinachofanyika ni kuyatoa na kuyasaga magamba kwa kile kinachoelezwa ni kutengeneza dawa za kuongeza nguvu za kiume na maradhi mengine.

Pia, hutumika kutengeneza mapamba kwa ajili ya matajiri kutoa zawadi kwa watu mbalimbali, na kwamba huhesabika kuwa ni matajiri kama wataweza kutoa zawadi ya magamba ya kakakuona.

Aidha, alisema takwimu zinaonyesha biashara ya meno ya tembo imepungua kwa kiasi kikubwa nchini, na kwamba hatua ya serikali kuimarisha mifumo na kuwachukulia hatua vinara wa biashara hiyo. Kwa mujibu wa Pius, takwimu zinaonyesha mwaka 2009 hadi 2013 asilimia 60 ya tembo waliuawa, na kati ya 142,785 waliokuwapo waliobakia ni 50,300.

Alisema awali biashara ya meno ya tembo na pembe za faru ilishika kasi kutokana na usimamizi dhaifu wa sheria na faini ndogo ambazo ziliwafanya wenye fedha kuzilipa kirahisi.

"Biashara hii inahusishwa kwa namna moja au nyingine na suala la ugaidi kwa kuwa wanauza pembe za ndovu na meno ya tembo wanapewa silaha, mfano ni nchini Congo ambako wanapeleka nyara hizo na kupata magari yenye silaha," alisema.

Kwa mujibu wa Pius, pia biashara hiyo inahusiana na biashara ya fedha chafu na kwamba ilikuwa ngumu kuidhibiti kutokana na wanaofadhili kuwa na nguvu kutokana na fedha zao.

"Biashara hii inafanywa na watu wenye fedha nyingi sana ambao hawapo hapa nchini, wanatoa fedha kufadhili hatua zote hadi kufika bandarini na nchi husika. Lakini kwa sasa tangu China imepiga marufuku biashara hiyo soko la meno na pembe imeshuka duniani," alibainisha.

Asilimia 32 ya eneo la nchi ya Tanzania ni ardhi iliyohifadhiwa, vilima vilivyohifadhiwa 25, maeneo yaliyochini ya hifadhi ya jamii (WMAs) yapo 38.

Aidha, Tanzania ina jumla ya hifadhi za taifa 21 zilizopo chini ya Shirika la Hifadhi ya Taifa (Tanapa) na kwa ujumla utalii unachangia asilimia 17 ya Pato la Taifa (GDP) inatokana na utalii na asilimia 25 ya fedha za kigeni zinatokana na utalii.

Alisema asilimia 80 ya utalii nchini ni wa wanyamapori, huku eneo la utalii wa asili halijafanyika inavyotakiwa.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya GF Trucks & Equipments Mehboob Karmali (kushoto), akiwaongoza wafanyakazi na marafiki katika futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugai: Masele acha fitina

**INATOKA UK. 2**

(Tanzania), kwa Katibu wa Bunge la PAP na Rais wa Bunge la PAP kwani tulitaka kuhakikisha anaipata.

"Kwa sababu ya unyeti wa hicho tunachomwitia nyumbani, kesho yake tukapeleka tena barua, keshokutwa (siku iliyofuata) tukampelekea taarifa tena hadi kwenye WhatsApp yake," Spika Ndugai alisema.

Ndugai alisema baada ya kupata taarifa hiyo, Jumatano ya wiki iliyopita, Masele alisimama kwenye Bunge la PAP na kusema licha ya kuandikiwa barua hiyo, Waziri Mkuu amemtaka aendelee na shughuli zake.

"Huyu ni kijana wetu, anaonyesha kwamba katika nchi ya Tanzania tuna migogoro mikubwa kiasi hicho ikiwamo baina ya Spika na Waziri Mkuu. Masele tumekuita kwa sababu ya mambo ya tabia mbaya za hapa nyumbani, habari za huko (PAP) mtajua wenyewe, hayatuhusu sisi," alisema Ndugai.

Aliongeza kuwa mambo yaliyokuwa yanasemwa na Masele yalikuwa yanatoa taswira mbaya kwa Tanzania katika Bunge hilo la Afrika.

**SHAURI LILIVYOKUWA**

Awali, akiwasilisha taarifa ya kamati yake kuhusu shauri hilo bungeni jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emmanuel Mwakasaka, alisema kamati yake imemkuta Masele na hatia na kupendekeza asimamishwe kushiriki mikutano mitatu ya Bunge kuanzia jana.

Mwakasaka alisema Mei 13, mwaka huu, Ndugai aliwasilisha shauri hilo na kamati yake ilipochunguza, ilibaini amekiuka masharti ya Kifungu cha 2(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Maadili ya Bunge kwa vitendo vyake vya kudharau mamlaka ya Spika, kudhalilisha Bunge na kuchonganisha viongozi, kutohudhuria baadhi ya vikao vya mkutano wa Bunge la Bajeti kwa kusafiri nje ya nchi bila kupata kibali cha maandishi cha Spika.

Alisema kamati ilitafakari uzito wa makosa ya shahidi yaliyofedhehesha Bunge, kugonganisha na kufarakanisha viongozi wa mihimili kuwa si vitendo vyema na pia ilizingatia kuwa ilikuwa mara ya kwanza kwa Masele kufanya makosa na kuletwa mbele ya kamati hiyo na kwamba ni mbunge kijana.

Kamati pia, alisema, ilizingatia Masele ni mwakilishi wa nchi katika PAP ambako si rahisi kupata nafasi ya uongozi kama anayoitumikia sasa.

**MASELE AJITETEA**

Mara baada ya azimio hilo kusomwa, Spika aliwaeleza wabunge kuwa ameandikiwa barua na Masele kuomba kuzungumzia jambo hilo bungeni, ombi ambalo aliliridhia.

Masele alipopata nafasi, alianza kwa kumwomba radhi Spika Ndugai, wabunge na viongozi wengine.

"Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kukuomba radhi wewe binafsi, wewe na familia yako kwa usumbufu wowote ambao umeupata kupitia sakata hili, lakini nitumie nafasi hii kuwaomba radhi wabunge wenzangu kwa usumbufu wowote ambao mmeupata.

"Nitumie nafasi hii pia kuwaomba radhi viongozi wangu wa juu akiwamo Rais wangu, Mheshimiwa John Magufuli, Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wetu wa wabunge wa CCM kwa usumbufu wowote ambao wameupata kutokana na jambo hili," alisema Masele.

Hata hivyo, Masele alisema angependa makosa yaliyoorodheshwa dhidi yake yawasilishwa bungeni ili wabunge na Watanzania wajue ukweli.

"Mheshimiwa Spika, barua hii nimeshika hapa imetoka Bunge la Afrika ya maombi ya mwaliko wa Stephen Masele kama Makamu wa Kwanza wa Bunge la Afrika kuhudhuria kikao cha Bunge ambacho mimi ninahusika na maandalizi ya Bunge hilo.

"Barua hii ni mawasiliano kati ya taasisi na taasisi ya Bunge la Afrika na Bunge letu na kwa utaratibu wa siku zote, kwa kupitia 'notification' hii ambayo ni rasmi inayotumwa kwa Katibu wa Bunge, sisi kwa taratibu zingine zote zinafuata na hii inasimama kama barua rasmi ya kusafiri," Masele alijitetea.

Alisema utaratibu wa Bunge ni kwamba wabunge hawaombi kibali hawaombi kusafiri bali wanatoa taarifa.

"Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, nilileta taarifa rasmi iliyoletwa na Bunge la Afrika kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge. Hata hivyo, tuhuma dhidi yangu zinasema nimesafiri bila ruhusa ya kibali chako, sisi tupo wabunge wanne wa Bunge la Afrika. Kwa nini Masele peke yake achukuliwe hatua na wabunge wenzangu wasichukuliwe hatua?

"Mheshimiwa Spika, kuna barua nyingine ambayo uliiandika tarehe 16, ikinisimamisha kuwa Mbunge wa PAP ambayo niliipokea saa 11 jioni kule nchini Afrika Kusini, nikiwa nasimamia vikao.

"Mheshimiwa Spika wangu, ninayekuheshimu, nilitafakari sana kwa haraka nifanye nini kwa maslahi ya taifa langu, nifanye nini kwa maslahi yangu binafsi kama kijana ambaye ninakua katika uongozi.

"Nilifikiria haraka na busara yangu ilniongoza, kama Spika wangu anaandika barua ya kunisimamisha bila hata ya kuniuliza, ananihukumu, basi nikate rufani kwenye chama changu (CCM), ndiyo sababu yangu ya kuwasiliana na viongozi wangu wa chama kwa maana ya Mwenyekiti wa CCM na Mwenyekiti wa Wabunge wa CCM ambaye ni Waziri Mkuu.

"Barua hii ilitaka kutumia kunichinja, kukata kichwa changu nisiwe Makamu wa Rais na nisiwe Mbunge wa PAP, kama angekuwa mtu yoyote, angefanya nini?... niliamua mimi kijana, wewe ni mzee wetu, kaka yangu, naamini mimi bado najifunza na wewe ungekuwa na nafasi ya kunilea kama ningekuwa nimekosea. Ungenipigia simu na kuniuliza 'Masele kuna kitu gani kinachoendelea huko?' Uliamua kunihukumu kabla hata ya Kamati ya Maadili haijaketi.

"Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninasikitika kwamba sikuchonganisha mihimili, bali nilikata rufani kwa chama changu kwa kuwa wewe ni mkuu wa mhimili huu... Waheshimiwa wabunge, kama mliona ile video, ilikuwa suala la sekunde tu, yule mheshimiwa ametaka kuniondoa kwenye madaraka, sikuwa na muda wa kutengeneza hotuba lakini niliamini kwa kuwa anatumia barua kutoka kwa Spika wangu, niliamua kusema nina sapoti ya serikali yangu," alisema.

Kwa sababu hiyo, mbunge huyo alimwomba radhi Spika Ndugai, akieleza kuwa hakuwa na lengo la kumvunjia heshima kiongozi huyo wa Bunge la Tanzania.

Masele aliomba kubatilishwa kwa ripoti ya Kamati ya Maadili kwa kuwa ina upungufu, lakini hoja hiyo haikukubalika kutokana na kutokidhi matakwa ambapo Spika Ndugai alisema Bunge haliwezi kuendeshwa kwa namna hiyo.

# Wambura mahabusu bado yamhusu

**INATOKA UK. 4**

na mawili ya kutakatisha fedha haramu.

Katika shtaka la kwanza ambalo ni la kughushi, mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Julai 6, 2004, sehemu isiyojulikana ndani ya jiji la Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa Wambura kwa nia ya kutapeli, alitengeneza barua ya kughushi ambayo haina kumbukumbu namba akionyesha imeandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Jeck System kuwa anadai kurejeshewa malipo ya mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba aliyokuwa ameikopesha TFF.

Katika shtaka la kutoa na kuwasilisha nyaraka ya uongo, mshtakiwa anadaiwa kutoa barua iliyokuwa haina kumbukumbu namba ya Julai 6, 2004, akijifanya kwamba ni barua iliyoandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Jeck System Ltd, akionyesha kuwa anadai mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba waliokopeshwa TFF huku akijua kuwa siyo kweli. Pia katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Wambura anadaiwa kutenda kosa hilo, Juni 17, 2015 katika ofisi za TFF, ambako kwa njia ya udanganyifu, alijipayia Sh. Milioni 10 kutoka TFF kwa kuonyesha kuwa ni sehemu ya malipo ya Dola za Marekani 30,000 pamoja na riba kutoka kwenye kampuni ya Jeck Systam jambo ambalo si kweli.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, Wambura anadaiwa kati ya Agosti 15 na Oktoba 21, 2014, makao makuu ya TFF alijipatia Sh. Milioni 25 kutoka TFF huku akijua fedha hizo ni zao la kosa la kughushi.

# Semina zilivyotafuna bil. 1.1/- Ngorongoro

**INATOKA UK. 2**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kemilembe Lwota, alisema licha ya ongezeko la watalii lililotangazwa na serikali, kamati yake hairidhishwa na kiwango cha ongezeko kutokana na wingi wa vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Pia aliitaka serikali kuhakikisha inawekeza vya kutosha katika sekta ya utalii badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

**BIASHARA WANYAMAPORI**

Awali, akiwasilisha hotuba bungeni kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, alisema serikali itaendelea kufunga biashara ya wanyamapori hai kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi.

Alisema serikali inakamilisha utaratibu wa kuwarejeshea fedha wafanyabiashara waliolipia kupata huduma mbalimbali zinazohusiana na biashara ya wanyamapori hai.

"Kwa sasa, wizara inandaa mkakati wa kitaifa wa biashara ya wanyamapori hai kwa njia ya ufugaji wanyamapori ili kuleta tija kwa wananchi na taifa," alisema.

Alisema mkakati huo utatoa fursa ya ajira kwa Watanzania pamoja na upatikanaji wa nyaraghafi kwa ajili ya viwanda vya ndani.

## HABARI KITAIFA

# Korti yataka Jamhuri kupeleka mashahidi kesi kigogo Takukuru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeutaka upande wa Jamhuri kupeleka mashahidi katika kesi inayomkabili Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai na wenzake ili washtakiwa wajue hatima yao kama kuachiwa huru ama kufungwa.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na mashtaka 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili mhasibu huyo.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, ilisema kesi hiyo ni ya muda mrefu washtakiwa wako mahabusu inatakiwa kusikilizwa imalizike.

"Washtakiwa wako mahabusu kesi ya muda mrefu leteni mashahidi washtakiwa wajue moja kama wanaachiwa au wanafungwa kuliko kuchelewesha usikilizwaji wake," alisema Hakimu Simba.

Awali Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Ipyana Mwakatobe, alidai kuwa waliwasilisha hati za wito kwa mashahidi lakini hajafika mahakamani.

Alidai upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kusikiliza ili waweze kuita mashahidi.

Wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, alidai kuwa Jamhuri iwataje majina ya mashahidi na wanatoka wapi.

Mwakatobe alidai mashahidi wanatoka mikoa ya Mwanza na Simiyu na kwamba tarehe itakayopangwa na mahakama mashahidi watakuwapo.

Hakimu alisema kesi hiyo itasikilizwa ushahidi wa Jamhuri Juni 3, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Upande wa Jamhuri umeshaita mashahidi 13 dhidi ya Gugai na wenzake.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo, ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo, makosa 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Katika kesi ya msingi, Gugai na mwenzake, wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume cha kipato chake, na inadaiwa alitenda kosa hilo kati ya Januari 2005 na Desemba 2015.

Inadaiwa akiwa Takukuru Dar es Salaam, Gugai alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake, huku akishindwa kuzitolea maelezo.



Wamachinga wakijiandaa kuhamisha kibanda chao kando ya barabara ya Bagamoyo, karibu na kituo cha daladala cha ITV, jijini Dar es Salaam juzi, ili kupisha katapila lililokuwa likisafisha eneo hilo, yakiwa maandalizi ya upanuzi wa barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tucta yaitaka Osha kumlinda mfanyakazi dhidi ya magonjwa

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi (Tucta), limetoa wito kwa uongozi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), kuendeleza jitihada za kumlinda mfanyakazi dhidi ya magonjwa, ajali na vifo vinavyoweza kusababishwa na mazingira ya kazi yasiyozingatia viwango stahiki vya kiusalama na afya.

Limeeza kuridhishwa na utendaji wa Osha katika kusimamia na kuwalinda wafanyakazi wanapokuwa kazini kupitia Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

Katibu Mkuu wa Tucta, Dk. Yahya Msigwa, aliyasema hayo katika salamu zake alizozituma kwa Osha hivi karibuni baada ya kuhitimishwa kwa maadhimisho ya siku ya Usalama na Afya mahali pa kazi duniani.

Alisema Osha imekuwa mstari wa mbele katika kuwalinda wafanyakazi wasidhurike wanapokuwa kazini, kwa kuhakikisha waajiri wanatekeleza Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

Alisema Watanzania wanajivunia uwapo wa Osha kwa kuwa mashirika na taasisi nyingi zimeanza kuwalinda na kuwajali wafanyakazi wao.

Dk. Msigwa pia aliupongeza uongozi wa Osha kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho ya siku ya Usalama na Afya mahali pa kazi duniani pamoja na ushiriki wao mzuri katika sherehe za Mei Mosi, zilizofanyika kitaifa mkoani Mbeya.

"Kwa niaba ya uongozi mzima wa Tucta na kwa niaba ya wafanyakazi wote nchini, nachukua nafasi hii kukupongeza kwa dhati wewe binafsi, Mwenyekiti wa Bodi na uongozi mzima wa Osha kwa maandalizi mazuri ya wiki ya Usalama," alisema Dk. Msigwa.

Alisema Osha ambao ni Wakala waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu) wamekuwa na dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

# Maelfu wakutwa na homa ya ini

**Na Mary Geofrey**

KATI ya wachangiaji wa damu 307,835, waliojitokeza kuchangia damu katika vituo mbalimbali nchini mwaka jana, watu 13,613 (asilimia 4.4) walibainika kuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina ya Hepatitis B na 1,092 virusi aina ya Hepatiti C.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura, virusi vya kundi B na C vinapoingia kwenye mwili wa binadamu kushambulia ini na baadhi hawaonyeshi, hupata athari kwenye ini na wengine kupata maambukizi sugu na wa muda mrefu.

Aidha, takwimu hizo zilieleza kuwa, katika kipindi cha mwaka juzi kati ya watu 233,953 waliojitokeza kuchangia damu, watu 11,417 (asilimia 4.9) walikuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina B.

"Katika jamii, utafiti mahususi ujulikanao kama 'This Tanzania HIV Indicator Survey' uliratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, mwaka 2016/17 ulionyesha maambukizi ya homa ya ina aina ya B ni asilimia 4 miongoni mwa Watanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49," alieleza Sungura katika taarifa hiyo.

Alisema virusi hivyo vya kundi B, C na D huambukizwa kwa njia ya kuongezewa damu yenye virusi vya ugonjwa huo, kujamiiana na wenye maambukizi na kujidunga sindano yenye virusi vya ugonjwa huo.

Alitaja njia nyingine za maambukizi ni majimaji yenye uambukizo kama damu na matapishi kutoka kwa mgonjwa mwenye virusi hivyo na kuingia kwa mtu mwingine andapo ana kidonda au michubuko ya ngozi.

Alisema njia zinazoeneza virusi vya homa ya ini ni zile zinazoeneza Ukimwi ikiwamo mama anapoweza kumuambikiza mtoto wakati wa ujauzito na kujifungia.

"Taarifa hii pia inabainisha na kufafanua ukweli juu ya ugonjwa huu kufutia taarifa potofu zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu ugonjwa huu na namna ya kujikinga," alisema Sungura. Kuhusu dalili za ugonjwa huo, alisema mtu anaweza kuugua na asiwe na dalili na hufanya hivyo pindi unapokolea mwilini ambazo ni mwili kuishiwa nguvu, kichefuchefu na kutapika, homa ya tumbo.

Alisema hatua zinazochukuliwa na serikali ni kutoa chanjo kwa watoto wadogo, kwa watu walio katika hatari ya kupata maambukizi na kwamba wameanza kutoa chanjo hizo kwenye vituo vya afya nchini.

# Same kupigwa jeki utunzaji misitu

SERIKALI imesema iko tayari kuendelea kutekeleza azma ya kuwasaidia wananchi wa kata za Bendera, Kihurio, Ndungu na Maore kuhusu shabaha yao ya kutunza misitu ya asili.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Same Mashariki (Chadema), Naghenjwa Kaboyoka.

Katika swali lake, Kaboyoka kama serikali iko tayari kuanzisha miradi ya utunzaji mazingira kwa kuwa wananchi wa jimbo hilo wako tayari kuanzisha misitu ya vijiji kwenye maeneo yenye ukame kama kata hizo ili kuhifadhi mazingira.

Akijibu swali hilo, Kanyasu alisema hali hiyo inatokana na ukweli kwamba pamoja na kuwa vijiji hivyo viko nyanda za ukame, bado vina uoto mzuri wa asili ambao ukitunzwa vizuri utasaidia kuboresha hali ya hewa, uhifadhi wa baionuai na huduma za kijamii kama maji.

Pia alisema Wilaya ya Same kiikolojia na kijiografia imegawanyika katika kanda kuu mbili, yaani ukanda wa milimani ambao hali yake ya hewa ni nzuri kulinganisha na ukanda wa tambarare ambapo hali ya hewa ni ukame.

"Kwa maana hiyo, kata zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ziko katika ukanda wa tambarare na kwa bahati nzuri zina uoto wa misitu," alisema.

Alisema wizara imeweka utaratibu wa kushirikiana na halmashauri za wilaya na wananchi katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa maliasili.

"Mathalan, katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, utunzaji wa mazingira umehusisha utoaji wa elimu kwa wananchi na kuanzisha Kamati za Maliasili na Misitu, kuandaa mipango ya usimamizi na kutunga sheria ndogo za usimamizi wa maliasili," alisema.

Vile vile, alisema kupitia utaratibu huo wananchi wanashirikiana na wizara na halmashauri kupanda miti kwenye maeneo ya wazi.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Hanang, Dk. Mary Nagu, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

## Mbunge wa CCM awashtaki polisi

MBUNGE wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, amesema wakati Jeshi la Polisi likitekeleza majukumu yake kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na hata uvunjaji wa katiba kwa kisingizio cha maagizo kutoka juu.

Akiuliza swali bungeni jana kutokana na madai hayo ya ukiukwaji wa sheria na haki za binadamu, Kachauka alihoji ni mamlaka gani zipo juu ya sheria.

"Je, maagizo hayo yanayopingwa na sheria za nchi na kukiuka haki za binadamu nini hukumu ya yule aliyetendewa kinyume cha sheria?" Alihoji.

Kuchauka pia alihoji: "Je, huyu anayekutwa na kadhia hii hana haki ya kumjua huyo mwenye mamlaka ya juu?"

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema jeshi hilo hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

"Kwa msingi huo Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 inampa mamlaka askari polisi kutumia nguvu ya wastani anapokuwa anatekeleza kazi yake kulingana na mazingira yaliyopo," .

Aidha, alisema hakuna mamlaka ya juu katika Jeshi la Polisi iliyo juu ya sheria kiasi cha kuvunja sheria.

Pia alisema nchi inafuata misingi ya demokrasia na utawala bora ambapo mtu yeyote anao uwezo wa kwenda kutoa malalamiko yake kwenye chombo chochote cha kisheria na hatua stahiki zikachukuliwa.

"Hakuna mamlaka inayomzuia mtu kumuona mtu ambaye anadhani atamsaidia kutatua tatizo lake linalomsibu," alisema Masauni.

# Bandari za Kigombe, Kipumbwi kurasimishwa

BUNGE limeelezwa kuwa Kigombe na Kipumbwi wilayani Muheza na Pangani ni miongoni mwa bandari 24 zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii na zimeorodheshwa kwa ajili ya kurasimishwa.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tanga Mjini (CUF), Mussa Mbarouk.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema katika kijiji cha Kigombe wilayani Muheza na Kipumbwi wilayani Pangani kuna bandari za kienyeji zinazotumika kwa uvuvi na kusafirisha abiria na bidhaa.

"Je, ni lini serikali itarasimisha bandari hizo kwa kujenga gati pamoja na kituo cha forodha?" Alihoji. Akijibu swali hilo, Nditiye alisema hatua inayoendelea hivi saa kuhusu bandari hizo ni kuzipanga katika madaraja ili kubaini zile ambazo zitachukuliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) moja kwa moja.

"Zitachukuliwa na TPA moja kwa moja kwa kuziendesha baada ya kuboreshwa na kuendelezwa kwa miundombinu yake ikiwamo kujenga gati na kuweka kituo cha Forodha. Ziko ambazo zitaendeshwa kwa mkataba na zile ambazo zitawekwa chini ya uangalizi wa halmashauri ya maeneo husika," alisema.

Alisema kazi hiyo inatarajiwa kukamilika kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2019/20 na baada ya urasimishaji huo usimamizi wa sheria na udhibiti wa maeneo hayo utafuata.


Awali, Nditiye alisema serikali ina taarifa ya uwepo wa bandari hizo bubu katika mwambao wa Pwani pamoja na changamoto za kiusalama, kiulinzi na kiuchumi zinazoletwa na bandari hizo.

"Ili kudhibiti matumizi ya bandari hizo, mamlaka zinazohusika na zimeelekezwa kushirikiana na kuweka mikakati pamoja ya kudhibiti matumizi ya bandari hizo," alisema.

Hata hivyo, alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kutambua bandari zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii ili kuzirasimisha kwa kuziweka chini ya uangalizi wa vijiji vilivyo kwenye maeneo husika.

Katika kutekeleza maelekezo hayo, alisema TPA ilikamilisha kazi ya kukusanya taarifa za Bandari Tanzania Bara na kubaini kuwa kuna bandari zisizo rasmi 208 katika mwambao wa Bandari ya Hindi.

"Baada ya kazi hiyo, TPA iliainisha bandari ambazo zinafaa kurasimishwa," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Wamiliki wa migodi ya madini ya Tanzanite wa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, wakiwa kwenye kikao cha kusikiliza changamoto na mafanikio yao kilichoandaliwa na Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), tawi la Mirerani jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# IFAD yaahidi kuendeleza ufadhili kilimo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MFUKO wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) umesema upo tayari kuongeza ufadhili katika kuendeleza miradi inayotekelezwa na programu ya miundombinu ya masoko na mnyororo wa thamani (Mivarf) nchini.

Hayo yalisemwa jana wilayani Karatu mkoani hapa na Rais wa Mfuko huo wenye Makao yake mjini Roma, Italia, Gilbert Houngbo, wakati alipotembelea na kukagua ghala la kisasa la kuhifadhi vitunguu maji, lililopo katika Kijiji cha Mang'ola, Tarafa ya Eyasi wilayani Karatu mkoani Arusha jana.

Alisema IFAD itaongeza fedha endapo Serikali ya Tanzania inataka mradi huo uongezewe fedha kwa ajili ya kuendeleza awamu ya pili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

"Nimeridhishwa na ubora wa mradi wa ghala hili na ni moja ya maghala bora ambayo sijawahi kuyaona katika maeneo ambayo IFAD inafadhili Afrika, hili ni ghala la mfano baadhi ya nchi zinazopata ufadhili wetu zinafaa kutuma watu kuja Tanzania na kutembelea ghala hili wajifunze," alisema.

Houngbo alisisitiza kwamba mfuko huo kama Serikali ya Tanzania itapendekeza kuongeza fedha, kusaidia miaka minne kwa ajili ya kuiwezesha Mivarf kuendeleza kazi zake ipo tayari.

Hata hivyo, alisema anatarajia kukutana na Waziri wa Fedha wa Tanzania na watendaji wa ngazi za juu katika wizara hiyo, mjini Dodoma kabla hajaondoka kurejea Roma kujadili suala hilo na mengine yanayohusu ufadhili wa mfuko huo nchini, katika sekta mbalimbali za kilimo.

Akitoa taarifa, Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alimshukuru Rais huyo wa IFAD, kwa kuiweka mbele Wilaya ya Karatu, katika kuipa

ufadhili wa utekelezaji wa miradi kwa manufaa ya wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema Mivarf ilianza utekelezaji wa miradi katika wilaya hiyo, mwaka 2013/2014 ya miundombinu ya masoko, barabara, uwezeshwaji wa wazalishaji na kuwaunganisha na masoko na mpango wa huduma za fedha vijijini.

Mahongo alisema Mivarf imefanikiwa kutekeleza miradi iliyogharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu.

Alisema Mivarf kwa ufadhili wa IFAD imejenga ghala la kisasa katika Kijiji cha Mang'ola Barazani, ambalo limegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.5.

Pia wamekarabati barabara yenye urefu wa kilomita 16 kutoka Kijiji cha Qand'dend hadi Dumbechand, ambayo imegharimu zaidi ya Sh. milioni 893.

Theresia alisema Mivarf pia imekarabati

barabara ya kutoka Mang'ola hadi Laghangarer yenye urefu wa kilomita 11, ambayo imegharimu zaidi ya Sh. milioni 654.

Alimweleza kuwa Mivarf imefanikiwa kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo namna ya kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi na kuwaunganisha na masoko ya zao la vitunguu na namna ya kuongeza zao hilo na mnyororo wa thamani, pamoja na kuwawezesha kupata bei nzuri katika masoko.

Mratibu wa Programu ya Mivarf kitaifa, Walter Swai, aliwataka wananchi ambako miradi hiyo imetekelezwa kuhakikisha wanaitunza

# Kesi ya anayedaiwa kukata watu masikio yaahirishwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KESI inayomkabili mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Anselm Minja ya kuwakata masikio watu wawili, imeahirishwa hadi Juni 21, mwaka huu, baada ya upelelezi wa ksi hiyo kutokamilika.

Kabla ya kuahirishwa Wakili wa Serikali, Ahmed Hatibu aliieleza Mahakama ya Wilaya ya Arumeru, mkoani hapa, kuwa upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo aliomba ipangwe tarehe nyingine.

Hatibu aliieleza mahakama hiyo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Amalia Mushi, kuwa upelelezi wa shauri hilo upo katika hatua za mwisho, ili mtuhumiwa aweze kusomewa maelezo ya awali.

Baada ya maelezo hayo Hakimu Amalia alimuhoji Wakili wa Utetezi, Innocent Mwanga, kama ana hoja ya maelezo yaliyotolewa na upande wa mashtaka na kusema hana pingamizi lolote.

Hakimu Amalia aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 21, mwaka huu na dhamana ya mtuhumiwa inaendelea.

Minja ambaye ni maarufu jijini hapa, anamiliki maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, alipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza Machi 28, mwaka huu, kwa kosa la kuwajeruhi watu wawili kwa kuwakata masikio ya kushoto na kuwasababishia ulemavu wa kudumu.

Alikamatwa Machi 27, mwaka huu na kulala rumande katika Kituo Kikuu cha

Polisi jijini hapa, kisha kufikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani hapa Machi 28, mwaka huu.

Alisomewa mashtaka yake na Wakili Mwandamizi wa Serikali Mkoa wa Arusha, Martenus Marandu mbele ya Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Obadia Bwegego na kudai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Julai 21, mwaka 2017 eneo la Njiro, huku akijua kuwa ni kinyume cha sheria.

Marandu aliwataja waliokatwa masikio ya kushoto kuwa ni Aloyce Petro na Samwel Sambeke ambao kwa sasa wamepata ulemavu wa kudumu na kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ya kujiingizia kipato.

Marandu alidai mahakamani hapo kuwa Minja alitenda ukatili huo wa kuwakata masikio raia hao, waadilifu kwa kutumia kisu kikali na kuondoa kabisa sehemu ya sikio kwenye miili yao.

# Wanafunzi 49 Sekondari Arusha DC hawajaripoti

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANAFUNZI 49 wa Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru mkoani hapa, hawajulikani walipo kutokana na kile kilichodaiwa wameshindwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza tangu Januari, mwaka huu.

Wakizungumza katika kipindi cha maswali na majibu katika kikao cha Baraza la Madiwani, Diwani wa Viti Maalumu (Chadema), Nuru Ndosi na Elinipa Laizer, walitaka kufahamu wanafunzi hao walipo na wanafanya nini na kwa nini hawakuripoti katika shule walizopangiwa.

Akijibu maswali hayo, Ofisa Elimu Sekondari kwenye halmashauri hiyo, Sophia Msophe, alisema, idadi ya wanafunzi ambao hawakuripoti shuleni ni 49, wanatoka katika shule mbalimbali za sekondari kwenye halmashauri hiyo.

"Mwenyekiti, wanafunzi wapo 49 wanatoka katika kata mbalimbali kwenye halmashauri yetu na Machi 30, mwaka huu, tuliandikia barua Tamisemi kuwajulisha idadi ya wanafunzi walioripoti na ambao hawakuripoti shuleni," alisema Sophia.

"Sheria inasema endapo mwanafunzi hajaripoti au kuhudhuria shuleni kwa kipindi cha miezi mitatu siku (90) jina lake linatakiwa kufutwa," aliongeza Sophia.

"Septemba mwaka huu, ulikuwa muda wa mwisho kuwasilisha taarifa za wanafunzi ambao hawakuripoti na tumeshapeleka majina yao, ili utaratibu wa kuwafuta unafanyike," alisema Sophia. Alisema kabla hajapeleka Tamisemi taarifa za watoto hao alizungumza na wenyeviti wa vijiji, watendaji wa kata kwa kushirikiana na wakuu wa shule hizo ili kufanya uchunguzi wanafunzi hao wamekwenda wapi kwa sababu hata mitaani hawaonekani.

"Septemba 9, mwaka huu, tuliwaandikia wakuu wa shule barua wazipeleke katika vikao vya kata 'ODC' na walijaribu kufanya uchunguzi na taarifa walizotuletea zinasema hawakupata majina ya wanafunzi hao na maeneo wanayoishi," alisema Sophia.

Alisema utaratibu uliopo wanafunzi watoro na ambao hawakuripoti shuleni majina yao yanaandikwa na kupelekwa katika ofisi za kata na vijiji, ili viongozi waweze kuwafuatilia kwa karibu.

Hata hivyo, alisema baada ya kufuatilia jambo hilo, waligundua tatizo la utoro linasababishwa na baadhi ya wazazi kushindwa kuwasomesha watoto wao na kukosekana kwa chakula shuleni.

"Ukosefu wa chakula umechangia utoro shuleni na tumejaribu kufuatilia shule chache, ambazo zinatoa huduma ya chakula vizuri, kimaudhurio ya wanafunzi yapo vizuri," alisema Sophia.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha DC, Noah Lembris, aliwataka madiwani wakati wanapokuwa kwenye mikutano yao, kata na vijiji wahamasishe wazazi kuchangia fedha za kununua chakula, ili kukabiliana na changamoto ya utoro shuleni.





# Upendeleo, ubinafsi vyatajwa sumu utoaji huduma kwa umma

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KATIBU Msaidizi Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Anna Mbasa, amesema upendeleo, ubinafsi na mihemko ya kisiasa ni miongoni mwa mambo yanayokwamisha utoaji huduma kwa wananchi.

Mbasa amesema hali hiyo imekuwa ikijitokeza pale viongozi waliopewa dhamana wanapotanguliza mbele maslahi binafsi.

Alikuwa akizungumza jana wakati akiwasilisha mada kuhusu mgongano wa maslahi kwa viongozi wa umma na binafsi kwa viongozi wa serikali mkoani Kilimanjaro.

Mgongano huo unaweza kutokea pale viongozi hao wanapotanguliza maslahi binafsi kwa kutumia madaraka kujinufaisha au watu walio karibu nao bila kujitazama jamii inayowazunguka.

Alisema hali hiyo inapotokea inachangia viongozi kuacha kutumia madaraka yao kwa kuwaletea wananchi maendeleo na badala yake kujenga mazingira ya wananchi kuichukia serikali.

"Mwananchi anafika katika ofisi yako anahitaji huduma, lakini hapati na badala yake unampiga tarehe na kutengeneza mazingira ya rushwa na viongozi wanawake mmekuwa mkidharauliana hasa pale unapoelekezwa jambo na mkubwa wako wa kazi. Tuache na kubadilika serikali ya awamu ya tano haitakubali hali kama hiyo.

"Viongozi tunao waraka kuhusu mavazi lakini inashangaza kuona viongozi wengine mnavaa nguo za ajabu hasa mnapokuwa ofisini. Unamkuta mwanamume amekuja vifungo vyote vya shati viko wazi au wadada mnakuja na nguo fupi ambazo si heshima na ukiambiwa mnaanza kunung'unika kwa maneno ya kejeli na dharau kwa viongozi wenzenu," alisema Mbasa.

Alisema hakuna utunzaji wa mali ya umma pamoja na viongozi kutembea na magari ya serikali usiku katika mambo binafsi, hali ambayo inasababisha wananchi kuona kuwa viongozi hao wanachezea rasilimali za taifa na matokeo yake wananchi kuichukia serikali yao.

Kuhusu suala la rushwa katika mkoa wa Kilimanjaro, alisema uchunguzi wao mdogo unaonyesha kuwa tatizo la rushwa na ukiukwaji wa maadili linafanywa na viongozi wa ngazi za juu wenye mishahara mikubwa.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Bwai Biseko, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alikiri kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa kimaadili katika mkoa huo ambapo tayari wanayafanyia kazi.

"Ni kweli tunapokea malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwa viongozi wetu na tunayafanyia kazi ila kupitia mafunzo haya tunatarajia mabadiliko makubwa ya kimaadili katika kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo katika serikali ya awamu ya tano," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akishiriki upakuaji wa mifuko 200 ya saruji jana, ambayo itatumika kufanya upanuzi wa Kituo Kikuu cha Polisi cha Wilaya ya Hai (Boma ng'ombe). **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Tume yaonya walimu walevi na mafataki

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI imesema siku za walimu wanaojihusisha na ulevi, utoro kazini na wale wanaojihusisha na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, zinahesabika. Kutokana na hali hiyo, Katibu wa Tume ya Utumishi ya Walimu (TSC), Wilfrida Gasper, ameonya baadhi ya walimu wenye tabia hiyo kujitathmini kabla ya kusubiri adhabu ikiwa ni pamoja na kufutwa kazi.

Alikuwa akizungumza jana na walimu wa shule za msingi na sekondari za wilaya ya Hai.

Alisema wako baadhi ya walimu ambao wamekuwa na tabia ya kujihusisha na vitendo vya mapenzi na wanafunzi, ulevi, kuvaa mavazi yasiyo staha na hata utoro shuleni, huku wakijua kufanya hivyo ni makosa Alisema: "Ualimu ni fani yenye heshima, wahusika wanatakiwa kwanza kujiheshimu, hatutegemei kutokea mtu asiyejiheshimu na akijiusisha na ulevi haipendezi. Walimu tunawaombeni sana msiwe mnawatamani wanafunzi kwani hao ni sawa na watoto wenu, wafundisheni ili waje kuwa walimu kama ninyi." Naye Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Hai, Julius Kakyama, alisema wataendelea kufuatilia walimu wenye tabia kama hizi na hawatasita kuwachukulia hatua za kisheria. Pia aliwataka walimu na wazazi kuwapo ushirikiana ili kuongeza ufaulu katika wilaya hiyo.

Alisema kuwa wazazi wengi hawana ushirikiano na walimu jambo ambalo halipendezi.

# Chama cha Mapinduzi Kilimajnaro yawasuta wapinzani

**Na Paul Willium,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewasihi wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro, kuacha kuviunga mkono vyama vya siasa vinavyohubiri ubaguzi wa kidini na ukabila, kwa kuwa haviitakii mema Tanzania.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, wakati wa hafla ya kumpokea aliyekuwa Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi, Degratius Mushi.

Mushi aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Moshi Vijijini na Diwani wa Kibosho Magharibi, alijiuzulu wadhifa huo Aprili 27, mwaka huu, na kujiunga na CCM.

Mabihya alisema viko baadhi ya vyama vya siasa nchini vimekuwa vikieneza ubaguzi na kuchochea mifarakano baina ya wananchi na viongozi wa serikali.

"Unapomuona mtu anaeneza suala la ubaguzi, unapaswa kumwangalia kwa umakini sana, maana haitakii mema nchi yetu.

Wako baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wamekuwa mstari wa mbele kueleza ubaguzi, sisi Watanzania ni wamoja, hivyo tunapaswa kuwapuuza," alisisitiza Mabihya.

Alisema serikali ya awamu ya tano itaendelea kuwatumikia wananchi wote bila kujali mwaka 2015 walikipigia kura Chama Cha Mapinduzi au la.

Katibu huyo alisema mwaka 2015, aliyekuwa Diwani wa Kata hiyo (Mushi) alikosea njia baada ya kukuta mlango umefungwa na kuamua kupitia dirishani akiwa na dhamira ya dhati ya kuwatumikia wananchi.

Kwa upande wake, Mushi alisema sera ya Chadema ni kuwadanganya Watanzania kuwa serikali yao hakuna kinachofanyika, huku mioyo yao ikiwasuta kwa kuwalisha dhambi Watanzania.

"Tulikuwa tukipita na kueneza siasa za uongo kuwa serikali haijajenga hospitali, barabara, wala kuwafikishia wananchi huduma za maji, lakini wakati huo huo tukiumwa tunaenda kutibiwa katika hospitali zilizojengwa na serikali na pia barabara za lami tunazopitia zimejengwa na serikali hiyo tunayoikashifu," alisema Mushi.

Alisema mwaka 2015 alitumia nguvu kubwa kuhakikisha Chadema inalinyakua Jimbo la Moshi Vijijini na kuahidi kuhakikisha jimbo hilo analirejesha CCM.

Kada huyo mpya wa CCM amemtumia salamu Mbunge wa Jimbo hilo, Anthony Komu, kuanza kuaga bungeni mapema.


Ukurasa 18

Ofisa Tasaf: Haya ndiyo maisha mapya tuliyoyaunda Njombe


Ukurasa 19

Mafanikio 10 sekta ya mifugo

# BUFE

Ijumaa Mei 24, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




## Panasonic yapiga 'stop' Huawei

Ukurasa 15




# Wilaya kongwe 'iliyokucha' kiuchumi inayofichwa na shida kubwa ya usafiri

**Na Sabato Kasika,** aliyekuwa Liwale

LIWALE ni jina kongwe katika maeneo au wilaya za mikoa ya kusini. Sifa hiyo kubwa bado ilikuwa inaangukiwa na kasoro kwamba 'hapajaendelea.'

Lakini, leo hii mtu akasimama katika fikra hiyo kwamba 'hapajaendelea', utakuwa umepotoka, maana pana sifa zote zinazostahili kuibebesha wasifu 'pameendelea.' Kwanini hivyo? Hapo kuna mengi, kasoro moja kuu. Kimsingi, mtu anapoingia kwa barabara ya vumbi itokayo Nangurukuru, umbali wa nusu kilomita kufika mjini, anaanza kuona mazingira yote ya mji na hapana shaka anakiri katika nafsi yake kwamba 'Liwale kumekucha.'

Ushuhuda unaokuwepo ni pamoja na mji kuzingirwa na miti mbalimbali, ikiwamo mikorosho, ambayo ni sehemu ya uchumi mkuu wa wilaya, zinaonekana nyumba mpya za kisasa zilizoezekwa kwa mabati ya kileo, nyingine vigae, lakini haziko mbali na baadhi ya nyumba kongwe zilizobeba viashiria vya Liwale ya zamani.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha


Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Mafanikio 10 sekta ya mifugo Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

**Kielezo**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Wasomi waanika njia ya kilimo ku Viwanda, wanahabari wadau rasn

• Vigingi vinavyokwamisha vyaorodheshwa

**Na Christina Haule, Morogoro**

SERA za masoko ya mazao nchini, zinanyooshewa vidole kuwa kikwazo kikubwa cha kilimo nchini licha ya kujitahidi kutumia mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha.

Hizo kimsingi ni fedha zinazohitajika kugharamia pembejeo na wamekuwa wakikosa masoko ya uhakika ya kuuzia bidhaa zao,hivyo wanashindwa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Haruni Mapesa, alisema katika mkutano wa pili unaojulikana 'Nkwabi Ng'wanakilala' ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Mtakatiu Mwanza cha jijini Mwanza, ukihusisha uandishi wa habari za uchunguzi na mazingira ya biashara uliofanyika mjini hapa.

Dk. Mapesa anasema, kwa ukosefu wa fedha za kulimia, pembejeo na hata kuvuna, si shida kwa wakulima kutokana na kuwapo mikopo inayotolewa na vikundi vikiwemo vyama vya kuweka na kukopa, vikoba na benki.

Katika maoni yake ni kwamba, wakulima kuwa na fursa kubwa ya kulima kibiashara ni tofauti na ilivyokuwa miaka ya zamani.

Anasema, kwa sasa wakulima wa mazao ya biasara wanakosa masoko ya uhakika na wanashindwa kumudu maisha, sambamba na kushindwa kurejesha mikopo, wakibaki na riba kubwa zinazoongezeka kila mara.

"Niliienda mkoani Ruvuma, nikakuta wakulima wamelima mahindi ya kutosha, nikiwahoji mbona sioni mkifanya biashara, wakasema wamezuiliwa kuuza nje ya nchi na serikali, ikanipa wakati mgumu kweli kuelewa tutafika wapi na suala la kilimo Tanzania?" anahoji Dk. Mapesa.

Anatoa mfano hai, wakulima mkoani Ruvuma wamekuwa wakiuza mazao yao katika nchi za Kenya, Malawi na Msumbiji na kupata fedha za kujikimu, pia kulipa ushuru unaosaidia serikali kufanya shughuli za maendeleo.

Mtaaluma huyo, anasema sera za masoko nchini bado zimebaki kuwa mwiba kwa wakulima, hata ikaua uzalishaji wa mazao kama vile mbaazi na korosho, ambazo kwa sasa zimeanza kupatiwa ufumbuzi wa masoko na huenda zikawa kimbilio cha wakulima.



Ofisa Uhusiano wa Bodi ya Korosho Tanzania, Bryceson Mshana (kulia), akisalimiana na wakulima wa korosho mkoani Morogoro, mara baa kuwatembelea na kuwapa elimu ya namna bora wanaweza kuongeza uzalishaji kwa kuzingatia kilimo bora.

> **Kazi ya vyama ni kuleta pamoja mazao ya wakulima ili wafanyabiashara wanunue moja kwa moja au kwa njia ya mnada.**

**WANAHABARI**

Mwanahabari mkongwe, Jenerali Ulimwengu, anasema suala la kilimo nchini linapaswa kupewa kipaumbele katika mazao yote, kama ilivyokuwa kwa katani zamani, ambayo iliainishiwa mikoa ya kulimwa kwa kuzingatia uwepo wa masoko na kufanya maendeleo kwa wakulima wa zao hilo.

Anasema katani ililimwa katika mikoa kama Morogoro na Tanga, huku ikisimamiwa kwa umakini wa kuhakikisha ubora wake unazingatiwa kuanzia katika ulimaji, mavuno na masoko yake.

Ushauri wake kwa serikali ni kwamba irejeshe hali ya mazao nchini ili kuwiana mwongozo wa kufikia hatma ya Uchumi wa



Wakulima wa alizeti wakiwa shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

BIASHARA

Panasonic yapiga 'stop' Huawei

Ukurasa 15

UCHUMI

Ofisa Tasaf: Haya ndiyo maisha mapya tuliyoyaunda Njombe


Ukurasa 18

BIASHARA

Mafanikio 10 sekta ya mifugo

Ukurasa 19

# ufikia Uchumi ni wa mkakati



da ya



Viwanda mwaka 2020, kama inavyokusudiwa, lakini kuna shaka ya kufikia iwapo hakutakuwapo maboresho ya sekta ya kilimo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, anaipongeza SAUT kupitia mradi wake wa 'Nkwabi Ng'wanakilala' ukihusisha uandishi wa habari za uchunguzi na mazingira ya biashara uliofadhiliwa na asasi ya Best Diology ya nchini Denmark na Umoja wa UIaya (EU).

Mtazamo wa mradi huo ni kuwaelimisha wanahabari, ili nao watoe elimu kuhusu utafiti unaotolewa na vyuo vikuu nchini, katika kukiinua kilimo kitaifa.

Anasema wanahabari wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo, na hivyo kushindwa kuwaunganisha wakulima na watafiti, na kwamba kupitia mkutano huo watatambua namna watakavyoweza kufanya habari za kiuchunguzi katika eneo la kilimo na kuifikishia jamii elimu hiyo kwa uweledi zaidi baada ya kutambua baadhi ya maneno magumu na misamiati ya masuala ya kilimo.

Balile anasema, ni vyema watafiti sasa nao wakawa karibu na wanahabari na kuwafafanulia na kuzungumza utafiti wao umebeba nini na unawezaje kuunganishwa na mkulima wa kawaida ukamuwezesha kupata soko na kufaidika toka kilimo cha kawaida kwenda kwenye kilimo cha kibiashara.

Anasema, suala la upatikanaji wa masoko kwa wakulima linapaswa kuwa wazi na huru ili kuwawezesa wakulima kuzitumia vyema tafiti wanazopewa na kuwaletea faida.

Balile ambaye pia ni mhitimu wa SAUT (wakati huo ikiitwa Nyegezi), anasema kuna wakulima wa nje ya nchi wanaolima kwa kuzingatia tafiti na kisha wanapata mazao bora na kuuza kwa bei kubwa, kiwafanya kilimo ili kiwaletee faida zaidi.

**WATAALUMA**

Makamu wa Mkuu wa SAUT-Mwanza, Profesa Costa Mahalu, anasema mchango wa wanahabari katika kusaidia kilimo ni muhimu, katika kusaidia kuwawezesha wadhamini kujua mahitaji ya wakulima na kuwasaidia.

Anasema, kwa kuzingatia umuhimu huo na taasisi za elimu ya juu nchini zikiwemo za kilimo, zinapaswa kuvitumia vyombo vya habari kufikisha elimu hiyo kwa walengwa ambao ni wakulima na kuwafanya wakulima waandae mazao bora, inayomletea tija ya kiafya na mapato mkulima.

Mkuu wa Kitivo cha Biashara wak SAUT, Dk. Anne Gongwe, anasema huo ni mpango unaowawezesha wanahabari kujifunza namna ya kutumia tafiti katika mazingira ya biashara.

Takwimu za kimataifa zinaitaja Tanzania kuwa katika nafasi ya chini, 139 duniani, katika kufanya biashara kwa urahisi. Hadi sasa SAUT imeshatoa mafunzo kwa wanafunzi wa habari zaidi 100, kufanya utafiti wa masuala ya kilimo biashara, katika miaka 15 ya mradi.

**MRATIBU MRADI**

Mratibu wa mradi, Judith Wanda, anasema lengo la mradi huo kitaifa ni kusaidia maboresho ya biashara, kupitia tafiti na mijadala inayomsaidia mkulima kupiga hatua katika maendeleo ya kilimo, kupitia tafiti zinazofanywa nchini.

Waziri wa Kilimo, Dk. Charles John Tizeba, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake latika mwaka wa fedha unaoisha, alisema sekta ya Kilimo imeendelea kuwa muhimu katika maendeleo ya uchumi wa wananchi kwa jumla, katika kipindi kilichopo mwelekeo ni kusaka Uchumi wa viwanda.

Inaelezwa kwamba, kilimo kinachangia asilimia 30.1 katika Pato la Taifa kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017, ikilinganishwa na asilimia 29.2 kwa mwaka 2016.

Akielezea mwelekeo wa malengo ya sekta ya Kilimo, Dk. Tizeba anasema, hadi kufikia mwaka 2025, yaanatazamiwa mageuzi kutoka kilimo cha kujikimu hadi kuelekea kibiashara.

Anasema, lengo la kuleta mageuzi yanayohakikisha kilimo kinakuwa chenye manufaa kwa nchi na wakulima, pia kuendana na dhamira ya Uchumi wa Viwanda, kuwa na hadhi kipato cha kati.

Kwa kumrejea Dk. Tizeba, kuna malengo yanayobadilisha kilimo katika mazao matano ambayo ni pamba, kahawa, tumbaku, chai na korosho, yatauzwa na kununuliwa kupitia vyama vya ushirika vya wakulima (AMCOS).

"Naomba ieleweke kwamba vyama vya ushirika siyo vitakavyonunua mazao haya, bali wanunuzi/wafanyabiashara ndio watakaonunua mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika," anasema Dk. Tizeba na kufafanua:

" Ni marufuku vyama vikuu vya ushirika au vyama vya msingi vya ushirika kupeleka dhana kwa wananchi kwamba vyenyewe ndivyo vinavyonunua mazao ya wanachama wake. Kazi ya vyama ni kuleta pamoja mazao ya wakulima ili wafanyabiashara wanunue au moja kwa moja au kwa njia ya mnada."

***Makala hii inatokana na maudhui ya Mkutano wa Pili wa Elimu ya Tafiti za Masuala ya Kilimo, Biashara kwa wakulima uliowashirikisha waandishi wa habari, wahariri na wataalamu kutoka vyuo mbalimbali nchini, uliofanyika mkoani Morogoro. Mwandishi wa makama anapatikana kwa simu: (+255) 0754654678***

# Panasonic yapiga 'stop' Huawei







Simu Panasonic. Picha ndogo ni simu ya Huawei. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KAMPUNI ya vifaa vya elektroniki ya Panasonic ya nchini Japan, imetangaza kusitisha biashara na kampuni ya Huawei, ikiwa sehemu ya kukidhi matakwa ya masharti ya nchi, katika biashara yake na Marekani.

Katika masharti hayo ni kwamba, bidhaa zozote zilizoundwa na vifaa asilimia 25 au zaidi kutoka Marekani ni hazitakiwi katika biashara.

Hata hivyo, kunaelezwa kuwapo utata kuhusu agizo hilo, kwa vile mtandao wa tawi la kampuni hiyo ya Panasonic nchini China, inayosema itaendeleza biashara na Huawei kama kawaida.

Ni hoja inayokuja wiki moja tu serikali ya Marekani, kuitangaza Huawei kuwa katika orodha ya kampuni ambazo haziwezi kufanya biashara nazo.

"Panasonic imetangaza katika taarifa za ndani kwamba, inasitIsha biashara na Huawei katika matawi yake yote 68, ambayo imezuiwa na serikali ya Marekani," imeeleza taarifa hizo.

Hata hivyo, hadi sasa haijaeleweka kama ni maamuzi ya kudumu au ya muda, kutegemea na maamuzi ya serikali ya Marekani kama yatabadilika.

Hivi karibuni, serkali ya Marekani ilitangaza kuizuia Huawei ambayo ni kampuni ya pili kubwa katika uzalishaji simu za mkononi duniani.'

Ni mambo yanayoendelea, huku kukiwapo msuguano na mvutano baina ya China na Marekani, wakiwekeana vikwazo vya ushuru wa kibiashara.

Ni muda sasa kampuni ya Huawei imekuwa mwathirika zaidi katika msuguano huo wa kibiashara baina ya China Marekani.

Serikali ya Marekani inayoinyooshea vidole Huawei kwamba inategemea serikali China, huku kampuni hiyo ikipinga kwa kauli, kwamba iko huru kibiashara. **BBC**

**BEI YA MAZAO** >> MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- **FEDHA** >> RAND 164.66 | KSH 22.75 | USH 0.61

UCHUMI

IJUE LIWALE

# Wilaya kongwe 'iliyokucha' kiuchumi inayofichwa na shida kubwa ya usafiri

**INATOKA UK.13**

- Wakazi kila kona nchini wakimbilia kuwekeza
- Wasimulia kilichowavuta; yupo aliyeapa 'siondoki'



Basi lililokwama eneo la Kimambi, Liwale. **PICHA: SABATO KASIKA**

Kadri mtu anavyozidi kuingia mjini kwa usafiri unaoenda taratibu kutokana na uhalisia wa barabara, hasa katika msimu wa mvua kama zinavyoendelea sasa, mwendo nao unakuwa taratibu zaidi, ushuhuda wa Liwale ni mjini unazidi kuongezeka.

Mengi yanayounda sifa ya mji yanazidi kuwa dhahiri: Bucha nyingi, shule kadhaa zilizoko jirani, maduka, maeneo ya starehe, soko kubwa, ofisi za umma kama vile Hospitali ya Wilaya, kituo cha polisi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Wilaya na idara zake mbalimbali, pia ofisi nyinginezo, ikiwamo benki.

Aidha, uchunguzi wa Nipashe mjini hapo, unagundua kuwapo mifugo mingi aina ya ng'ombe na wengine wanapatikana kwa wingi mahali hapo, sababu kuu ni kuwapo kwa wafugaji kutoka kanda ya ziwa walioweka makazi yao. Ni hali tofauti na wilaya nyingi za mikoa ya Lindi na Mtwara.

Hiyo imefanya, bei ya nyama ya ng'ombe kuuzwa kwa wastani wa Sh. 7,000 kwa kilo, tofauti na wilaya kama Ruangwa, ingawa zote ziko Mkoa wa Lindi. Huko, Nipashe ilishuhudia nyama ikiuzwa kwa bei si chini ya Sh. 9,000 kwa kilo.

Ushuhuda mwingine wa kushamiri Liwale kiuchumi ni kwamba, mtu anapokuwa mjini anaona biashara ndogo pamoja na wachuuzi wake waliosambaa kila kona, kama ilivyozoeleka katika mji mingine.

Hata hivyo, kuna wasifu mmoja unaoitenganisha Liwale na baadhi ya miji mingine inayokua kwa kasi kama vile Masasi mkoani Mtwara na Ruangwa, Lindi. Ni kwamba, hakuna jengo la ghorofa, ambayo mara nyingi ni kigezo cha mji kukua.

**UCHUMI ULIVYO**

Je, uchumi wake ukoje? Mfanyabiashara Mika Mgumbu, aliyezungumza na Nipashe, ana ufafanuzi ufuatao: "Liwale ni wilaya inayofaa kwa watu wa shughuli mbalimbali, wakiwamo wakulima, wafanyabiashara na wafugaji, lakini tatizo kubwa ni ubovu wa barabara kuu zinazoingia humo".

Mgumbu, anayejitambulisha kuwa mwenyeji wa Dodoma, aliyejikita katika biashara ya kuuza mahindi, unga na bidhaa nyingine nyingi mjini Liwale, anaelekeza sehemu kubwa ya lawama zake, katika miundombinu duni ya usafiri.

Akizungumza na gazeti hili safarini kutoka Liwale, ana mengi anayofafanua kuhusu wanavyokwama wafanyabiashara kutokana na adha ya miundombinu duni ya usafiri, huku akirejea tukio la basi alilokuwa akisafiria kukwama katika tope zaidi ya saa moja, eneo la Kimambi, likitoka Liwale kuelekea Dar es Salaam. Chanzo ni mvua zinazoendelea kunyesha.

> **"Wakati mwingine mtu anaweza kulazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam, kufuata bidhaa kipindi cha mvua, unajikuta ukikwama njiani hata siku nzima...**

Mgumbu anasema, Liwale imejaa wakazi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi waliofuata fursa za kiuchumi, zikiwamo za kilimo, biashara na ufugaji.

"Tatizo kubwa ni ubovu wa barabara, hasa wakati wa mvua, kwani kila mwaka ni lazima abiria au watu wenye usafiri binafsi wakwame njiani, wawe wanatoka Liwale kwenda maeneo mengine au wanaingia," anasema.

Anaamini, ni hali inayoweza kuchangia kuwafanya baadhi ya watu wanaotamani kuwekeza Liwale, waogope kufanya hivyo, sababu ni ubovu wa barabara.

"Liwale ya sasa imejaa wafanyabiashara, wakulima, wafugaji wa ng'ombe kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, ingawa kuna changamoto ya ubovu wa barabara ya kuingia au kutoka," anasema.



Sarah Chiwamba,Mkuu wa Wilaya ya Liwale. **PICHA: MTANDAO.**



Meneja wa Tanroads, Mkoa wa Lindi, Mhandisi Isaack Mwanawima. **PICHA: MTANDAO.**

Anaeleza kuwa, barabara itokayo Nangurukuru wilayani Kilwa hadi Liwale, yenye urefu wa kilomita 230, haina lami na wakati wa mvua, usafiri unakuwa wa shida, hali inayowaingiza wafanyabiashara katika zama ya hasara.

Nangurukuru ni eneo la njia panda inayounganisha barabara kutoka Dar es Salaam, Kilwa Masoko, Lindi na Liwale.

Mgumbu anaendeleza ufafanuzi:"Kwa ujumla ni kwamba, barabara zote mbili zinazoingia Liwale za kuelekea Nachingwea na ya Nangurukuru hazina lami na zimekuwa na usumbufu mkubwa wakati wa mvua za masika."

Judith Mhando, ni mfanyabiashara kutoka Tanga, aliyeweka makazi ya kibiashara mjini Liwale, bidhaa zake kuu zinajumuisha khanga, maduka ya nguo, vipodozi, bucha za nyama.

Anafafanua kwamba, mtu anapoenda mjini Liwale ni vigumu katika msimu wa mvua kwa kuwa kuna changamoto ya usafiri wakati wa kiangazi.

"Wakati mwingine mtu anaweza kulazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam, kufuata bidhaa kipindi cha mvua, unajikuta ukikwama njiani hata siku nzima...hii ndio changamoto ya huku," anasema Judith.

Judith anasema ataendelea kuishi mjini Liwale, kutokana na kile anachokitafsiri 'ameshaonja fursa' na anaamini kwamba kuna wakati barabara hizo zenye changamoto zitawekewa lami.

"Ukitaka cha uvunguni sharti uiname. Hivyo na mimi ninaendelea kuvumilia changamoto hizi, kwani ninajua kwamba chenye mwanzo hakikosi mwisho, kwa hiyo ipo siku zitaisha tu," anasema.

**DC LIWALE**

Sarah Chiwamba, ni Mkuu wa Wilaya ya Liwale, anayekiri ubovu wa miundombinu ni changamoto kwa wananchi wake. Imani yake ni wilaya itafunguka kibiashara na kiuchumi, kwa kuimarishwa mtandao wa barabara, zitakazoiunganisha na wilaya jirani na taifa.

"Naamini barabara hizi zikikamilika, wilaya hii na Mkoa wetu utaendelea kiuchumi, kwani suala la miundombinu ya barabara imekuwa kilio cha muda mrefu katika wilaya yetu", anasema Sarah.

Anafafanua kuwa, wakazi wengi wa wilaya hiyo ni wakulima, hivyo wanategemea barabara kusafirisha mazao yao ya korosho na ufuta, yanayozalishwa kwa wingi, kuelekea maeneo mbalimbali ya nchi.

Anadokeza, pia wanalima mbaazi na sasa wameanza kilimo cha alizeti, ambacho kimeonyesha matokeo mazuri na miaka michache anatarajia itakuwa na umaarufu mkubwa Liwale.

**TANROADS MKOA**

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Mkoa wa Lindi, Mhandisi Isaack Mwanawima, anasema wilaya zake za Liwale, Nachingwea na Ruangwa, bado hazijaunganishwa kwa barabara ya lami.

'Suala la ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami lipo, ili kufungua fursa mbalimbali katika mkoa. Ila kwa sasa, siwezi nikasema ni lini, kwa sababu ujenzi una taratibu zake, gharama na mambo mengine ya msingi," anasema.

Mhandisi Mwanawima anasema, ni muhimu kupitia Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003, kwa ajili ya kupata mwongozo wa utekelezaji majukumu yao, ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Anasema, barabara itokayo Nangurukuru hadi Liwale na Liwale hadi Nachingwe, zitaendelea kuboreshwa kadri inavyowezekana, wakati taratibu nyingine za kuweka lami zikiendelea kufanyika.

"Kwa sasa barabara hiyo inaboreshwa kuanzia Nangurukuru kwenda Liwale. Kwa wale waliopita huko hivi karibuni, watakuwa wameshuhudia jinsi kazi inavyoendelea, ili kuhakikisha inapitika bila usumbufu," anasema.

Mhandisi Mwanawima, anasema anatambua changamoto ambazo wakazi wa Liwale na Nachingwea wamekuwa wakikumbana nazo, wakati wa masika kwa kuzingatia kwamba umbali wa kutoka Nangurukuru hadi Liwale ni kilomita 230, wakati kutoka Liwale hadi Nachingwea ni kilomita 129.

**ILIKOTOKEA LIWALE**

Bakari Chikojo, mkazi wa Liwale ana simulizi kuwa ni sehemu ya kiutawala ya Wilaya ya Nachingwea, katika Mkoa wa Lindi, kisha Julai 12 mwaka 1975, ndipo ilitangazwa na kuzinduliwa rasmi kuwa wilaya.

Mkazi huyo wa mjini Liwale, anasema ni miongoni mwa wilaya kongwe nchini, kwa kuzingatia kwamba ilianzishwa miaka 14 tu baada ya uhuru wa Tanganyika, sasa ikitimiza miaka 44.

"Hata hivyo, miaka 44 tangu kuanzishwa kwake, barabara kuu zinazoingia wilayani kwetu zimekuwa ni changamoto kwa wasafiri kutokana na ukosefu wa lami, hali anayosababisha wateseke wakati wa mvua," anasema Chikojo.

Chikojo anasema, ni kawaida abiria kukwama njiani muda mrefu wakati wa mvua, magari yakinasa katika matope, hali inayochangia wao kuchelewa kufika safari zao.

# Biashara katika picha



Meneja Afya, Usalama na Mazingira wa kampuni ya Tanga Cement (TCPLC), Emmanuel Ntoma (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa mifuko 300 ya saruji yenye thamani zaidi ya Sh. milioni 3 kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Holili, Paschal Ntomola (kulia) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa, Ofisi 2 na nyumba 2 za walimu wa Shule ya Msingi Holili, iliyopo wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro katika hafla iliyofanyika kiwandani hapo, Pongwe, Tanga jana. Wa (pili kulia) ni Ofisa Mtendaji wa kata ya Holili, Fadhili Buzebuze na wengine ni maofisa wa kampuni hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa mikate akiwa ameisheheni kwenye pikipiki yake, wakati akisaka wateja katika eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Mkazi wa jiji akitafuta chupa tupu za plastiki kwa ajili ya kwenda kuziuza ili ajipatie riziki, katika eneo la Kigogo Luhanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

UCHUMI

# Ofisa Tasaf: Haya ndiyo maisha mapya tuliyoyaunda Njombe



Mnufaika wa Tasaf wilayani Wanging'ombe, akiwa katika nyumba yake mpya. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii(Tasaf), awamu inayotekeleza katika mpango wa kunusuru kaya masikini, uliozinduliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk.Jakaya Kikwete mwaka 2012 na utekelezaji kuanza mwaka 2013.

Lengo kuu ni kupunguza umasikini na kuongeza kipato cha kaya, kuziongezea uwezo wa kujimudu mahitaji ya msingi, chakula, malazi na mavazi.

Katika utekelezaji wake, kaya hupokea ruzuku zinazotofautiana, kulingana na idadi ya watu waliopo katika kaya na changamoto zao, ruzuku ambazo hupewa katika kipindi cha kila miezi miwili miwili.

**KUTOKA MAKAMBAKO**

Ofisa Mfuatiliaji wa Miradi ya Tasaf katika Halmashauri ya Mji Mdogo wa Makambako na Wanging`ombe, Edwin Mlowe, anasema shughuli nyingine inayofanywa na mfuko huo ni kuboresha miundombinu.

Kazi hiyo inafanywa kwa kuboresha miundombinu ya shule, hospitali na nyinginezo zinazofanana, ikiwamo kuchimba visima vya maji.

Anasema shughuli ya tatu ambayo Tasaf inaifanya, ni kuunda vikundi vya kuweka na kukopa kwa walengwa waliopo katika kaya masikini, zinajiunga katika vikundi, wanajiwekea zinawasaidia kuwekeza katika miradi midogo ya uzalishaji.

> **Lengo letu kubwa kuhakikisha tunakomesha changamoto ya umasikini. Tunaona matunda kwa sasa, hali ya umasikini katika kaya zilizopo katika mpango imeanza kwisha.**

"Inawezekana kikundi kikajiunga kwa ajili ya kuanzisha mradi wa mboga au ufugaji wa kuku, kilimo, lakini na shughuli nyingine mbalimbali ambazo zinaweza kuongeza kipato cha uchumi wa kaya na kikundi kwa ujumla," anasema Mlowe.

Anataja nyingine inayofanywa na Tasaf ni kujenga uwezo wa kutoa mafunzo ngazi zote za utekelezaji kuanzia mwananchi aliye katika kaya masikini na kamati, zinazosimamia walengwa na miradi yote inayoendeshwa na mfuko huo, pamoja na shughuli za walengwa.

Mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kusimamia kwa ufasaha miradi mbalimbali inayoendeshwa na Tasaf.

"Lakini kuna mafunzo ambayo pia yanatolewa katika ngazi ya kata hadi halmashauri. Wataalamu kutoka Tasaf, nao hupatiwa mafunzo kwa namna mbalimbali kwa ajili ya kuwawezesha kusimamia miradi kwa weledi zaidi," anasema Mlowe.

Pia, anafafanua kuwa miradi mingine inatekelezwa kupitia ufadhili wa Umoja wa Nchi Zinazouza Mafuta Duniani (OPEC), ambayo katika awamu ya kwanza na ya pili, ilijikita kutekeleza kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini awamu ya nne inatekeleza miradi katika mikoa wa Njombe na Arusha.

"Kimsingi katika miradi hii ya OPEC tunafanya kazi kuu nne ikiwamo ya kuboresha miundombinu katika sekta ya elimu na afya kwa kujenga madarasa, nyumba za walimu, Zahanati majengo ya utawala,"anasema mlowe na kuongeza"

"Pia tunajishughulisha na ajira za muda ambapo walengwa wa kaya masikini hujishughulisha na ajira za muda kupitia miradi mbalimbali inayosimamiwa na Tasaf," anasema.

**AJIRA**

Mlowe anasemna huko Makambako, wanatoa ajira za muda zinazotekelezwa kwa walengwa na mpaka sasa zimefika katika halmashauri 44, huku katika ajira za muda zinazofahiliwa na OPEC, zipo katika halmashauri 13, sita zikiwamo mkoani Njombe.

"Na tumekuwa tukifanya kazi kubwa ya kuhamasisha vikundi vya kuweka na kuwekeza kwa walengwa ambapo kila kijiji chenye mradi, tumekuwa tukiwagawanya walengwa katika vikundi mbalimbali na hujiwekea fedha kulingana na namna katiba zao zinavyowaongoza na kukopesha kwa ajili ya kuwekeza katika miradi midogo na wakizirejesha katika kikundi, kinapata faida na kukua," anasema Mlowe.

"Kwa sababu tunataka walengwa wote wajikomboe kiuchumi, huwa tunawahamasisha kwamba riba zisiwe kubwa, ili wamudu marejesho na kila mmoja akope kwa sababu walio wengi ni wazee hawawezi kuzalisha kipato kikubwa sana," anasema.

**MIRADI MINGINE**

Mlowe anataja miradi mingine inayoendeshwa na Tasaf kupunguza umasikini, ni kufuga mbuzi, kuku na ng`ombe na nguruwe kwa walengwa wa kaya masikini, ambayo inawasaidia kuongeza kipato.

"Lengo la Tasaf ni kutaka kuona hawa watu wanajimudu kabisa na tunapowapatia miradi kama hii ya ufugaji, huwa tunawapatia chakula cha kuanzia pamoja na huduma ya kiafya kwa mifugo husika kwa kipndi cha miezi miwili ya kwanza na baada ya hapo wanatunza wenyewe,"anasema Mlowe.

"Tunaona kwamba, kwa sababu walengwa wengi ni wazee, ni rahisi kuwapatia miradi hiyo ya mifugo kwa kuwa inakuwa katika mazingira ya nyumbani na ambayo ni rahisi kuihudumia na gharama zake ni nafuu," anafafanua

Jingine kwa mujibu wa Mlowe, wanawajibika kuwatafutia wataalamu wa mifugo, kwa ajili ya kuwasaidia pale wanapopata matatizo kiafya.

Anasema, kutokana na miradi hiyo mbalimbali inayoendeshwa na Tasaf kwa lengo la kupunguza umasikini nchini, tayari imeshaanza kuzaa matunda.

Pia, anasema Tasaf imekuwa ikifanya tathmini kutembelea walengwa hao na miradi wanayoitekeleza, ili kubadilisha maisha ya kikundi chao.

"Lengo letu kubwa kuhakikisha tunakomesha changamoto ya umasikini. Tunaona matunda kwa sasa, hali ya umasikini katika kaya zilizopo katika mpango imeanza kwisha.

"Hali zao zimeboreka na kupitia mafunzo mbalimbali ambayo tumekuwa tukiwapatia wamehamasika na wanafanyakazi kwa bidii kubwa," anasema Mlowe na kuongeza:

"Tunashuhudia hadi sasa mtazamo kwa wananchi wengine ambao siyo masikini umebadilika zamani walikuwa wanawaona kama watu wa chini sana ambao hawawezi chochote.

"Walikuwa wanawaita majina mbalimbali, lakini kwa sasa wanawaona wa maana sana. Hii yote imetokana na kujituma kwao ambako wamefundishwa na kuwezeshwa na TASAF."

Ahadi yake ni kwamba, Tasaf itaendelea kuhakikisha wanasimamia miradi yote inafanya kazi ya kumaliza umasikini kwa kaya.

FEDHA >> USD 2,300.96| Pauni 3,011.73| Euro 2,595.25

UCHUMI

# Mafanikio 10 sekta ya mifugo

**Na John Mapepele**

WAKATI serikali ikiendelea kufanya mabadiliko makubwa ya utendaji yenye nia ya kuinua uchumi hasa wa viwanda. Sekta za mifugo na uvuvi zimeanza kutoa matumaini katika kufanikisha dhamira hiyo.

Ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa fedha , julai 2018 hadi Mei 2019 Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina , anasema taasisi, bodi na wakala zilizopo zimetoa gawio kwa serikali kwa mara ya kwanza, ya thamani Sh.milioni 520.

Aidha, anasema katika mwaka huo, taasisi, bodi na wakala zake zimetoa mchango wa Sh. 411,793,383 kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii na kukarabati miundombinu muhimu ikiwamo majosho; kuchimba visima vya maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo; kujenga kituo bora cha kukusanyia maziwa; ununuzi wa zana za uvuvi; ukarabati wa masoko na mialo; na kusaidia vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi.



Shughuli za uvuvi zikiendelea.

### MAENEO ILIKOSAIDIA

Mosi, waziri anataja ni uanzishwaji Dawati la Sekta Binafsi lililozinduliwa Oktoba Mosi, mwaka jana, ili kufuatilia kwa karibu changamoto zinazoikabili sekta binafsi (Mifugo na Uvuvi), ufumbuzi na kuongeza uwekezaji na uchangiaji Pato la Taifa, katika safari iliyopo kuelekea Uchumi wa Viwanda.

Waziri Mpina anasema, dawati limesaidia kutatua migogoro ya kampuni za sekta binafsi na taasisi za serikali na imeharakisha upatikanaji wa huduma zilizokuwa zinachelewesha ufanisi wa kampuni hizo.

Aidha, inaelezwa imesaidia kuunganisha kampuni zinazohitaji huduma ya mikopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia utayarishaji wa Andiko la Biashara (Bankable business Plan).

Inaelezwa, jumla ya kampuni tano zimefaidika na huduma ya dawati kwenye huduma ya maandiko ya biashara. Hadi kufikia Aprili 2019, dawati limewezesha mikopo ya Sh. bilioni 17.3 na kuna mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 55, inategemewa kutolewa wakati wowote (Mifugo Sh. bilioni 26 na Uvuvi Sh. bilioni 29).

Dawati limewezesha Wizara kuingia katika makubaliano (MoU) na Viwanda Vinne vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika. Lengo ni kuongeza usindikaji maziwa kutoka lita 154,100 hadi 284,500 kufikia Desemba 2019.

Inalaezwa pia, dawati limetembelea na kukutana na wadau 213 wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kuwapa ushauri wa kitaalam. Wadau waliotembelewa ni pamoja na viwanda vya kusindika samaki, nyama, ngozi, maziwa, kuku pamoja na wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa.


Bidhaa za uvuvi zikiandaliwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Pia, waziri anasema Dawati la Sekta Binafsi wizarani inaendelea kuunganisha vyama vya ushirika 86 vya wavuvi na taasisi za kifedha, ili waweze kupata mikopo na kuanzishwa na vyama vya ushirika vipya vitatu katika wilaya za Chato, Ilemela na Tanga Mjini.

Pili, anasema wamepitia orodha ya tozo na ada zinazotozwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Taasisi zake na Wizara nyingine chini ya Sheria mbalimbali za mifugo na kubaini baadhi ya tozo na ada hizo kuwa ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya Sekta ya Mifugo kwa ujumla.

Katika mwaka ujao wa fedha, anasema wizara inapendekeza kuziboresha ili kuondoa usumbufu kwa wafugaji na kuongeza mapato katika sekta ya mifugo. Jumla ya Tozo 10 zimependekezwa kufutwa, iruhusu bidhaa za maziwa, nyama na kuku.

Pia, kuandaliwa kanuni chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya Mwaka 2008.

> **“Dawati limesaidia kutatua migogoro ya kampuni za sekta binafsi na taasisi za serikali na imeharakisha upatikanaji wa huduma zilizokuwa zinachelewesha ufanisi wa kampuni hizo.**

Hiyo inahusu kanuni za: Uogeshaji Mifugo; Uzalishaji, Uingizaji, Usambazaji na Uchanjaji wa Mifugo; Uhimilishaji, uhawilishaji kiinitete na Matumizi ya Madume Bora ya Mifugo; Kanuni ya Vitotoleshi na Kuku Wazazi; na Ukamataji wa Mifugo

Tatu, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya Ndani, Viwanda na Biashara (TBS), Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, Walemavu na Watoto (TFDA), Ofisi ya Rais) na OR-TAMISEMI imeendesha doria maalum ikiwa na malengo yafuatayo kudhibiti ukwepaji wa kulipa maduhuli ya serikali kwenye biashara ya mifugo na mazao yake, unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu;

Pia inaangalia kulinda viwanda vya ndani kwa kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa mbalimbali kinyume cha sheria, kanuni na taratibu; na kuwalinda wananchi/walaji dhidi ya bidhaa zisizokidhi viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Waziri anasistiza kwamba kabla ya operesheni hiyo kulikuwa na wastani wa makusanyo kwa mwezi Sh.1, 147,592,640.47, wakati baada ya operesheni wastani wa makusanyo yamekuwa Sh. 3,139,309,528 kwa mwezi.

Hii ina maana kuwa bila udhibiti huu, Serikali imekuwa ikipoteza wastani wa Sh. bilioni 2 kwa mwezi.

Nne, Wizara imetatua migogoro kadhaa na mingine ipo katika hatua mbalimbali. Wizara ilifanya kazi katika Wilaya za Uvinza, Kasulu na Kibondo (Kigoma); Tang-

INAENDELEA UK.20

# Mafanikio 10 sekta ya mifugo



Mfugaji ng'ombe akiwa katika nyendo zake. **PICHA: MTANDAO.**

**INATOKA UK.19**

anyika na Mlele (Katavi); Kalambo, Nkasi na Sumbawanga (Rukwa); Chunya na Mbarali (Mbeya); na Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Kisarawe (Pwani), ambapo migogoro 27 kati ya 43 sawa na asilimia 59.26 ilitatuliwa.

Wizara imetenga jumla ya hekta 350,576.05 kutoka katika maeneo yake ya vituo vya kupumzishia mifugo, Ranchi za Taifa, Mashamba ya TALIRI na Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs) ili yatumiwe na wafugaji kwa utaratibu maalum. Pia, Halmashauri za Tunduru, Mpanda, Biharamulo, Muleba na Kyerwa zimetenga jumla ya hekta 199,827.3 kwa ajili ya malisho ili kupunguza migogoro.

Wizara pia imeanzisha Kurugenzi kwa lengo la kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, vyanzo vya maji kwa mifugo na rasilimali za vyakula vya mifugo na hivyo kusaidia katika utatuzi wa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi. Katika hili Waziri Mpina anatoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Agizo alilolitoa tarehe 15 Januari, 2019 kwa Mawaziri nane (8). Agizo hilo lilihusisha OR – TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maliasili na Utalii; Maji; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kushirikiana kwa pamoja kufuatilia migogoro iliyopo na kuitafutia ufumbuzi.

Tano, Wizara imetekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kampeni ya uogeshaji. Kabla ya uzinduzi wa kampeni hii, kiwango cha uogeshaji kwa mwaka kilikuwa ni asilimia 10. Baada ya uzinduzi wa Kampeni ya uogeshaji mwezi Desemba, 2018, jumla ya michovyo 40,352,228 imefanyika, sawa na wastani wa michovyo 10,145,457 kwa mwezi. Hivyo uogeshaji mifugo umeongezeka hadi kufikia asilimia 25 kwa mwezi, ambalo ni ongezeko la asilimia 15.

> **"Viwanda vya nyama vya SAAFI (Rukwa), Tanganyika Parkers (Shinyanga na Mbeya) na Kiwanda cha maziwa cha Utegi na Musoma Dairy. Serikali inatafuta wawekezaji mahiri wa kuvifufua na kuviendesha viwanda hivyo.**

Alisema hadi kufikia mwezi Machi 2019, majosho yaliyopo ni 2,533, yanayofanya kazi ni 1,486 na mabovu 1,047. Mahitaji ya awali ya majosho ni 3,788 na hivyo kufanya upungufu kuwa 1,255. Wizara inaendelea kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya majosho nchini ambapo alisema katika mwaka 2018/2019 Wizara inakarabati majosho 161 kwa gharama ya Sh.235,113,200 katika mikoa 21 nchini.

Aidha, Wizara imehamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukarabati majosho ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya majosho 151 yalikuwa yamekarabatiwa. Wizara inazitaka Halmashauri zote kutekeleza Agizo la Chato la kukarabati majosho yote ifikapo mwezi Juni, 2019.

Waziri Mpina amesisitiza kuwa Halmashauri ambazo hazitatekeleza agizo hili zitanyang'anywa mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake.

Sita, Wizara kupitia NARCO imesaini Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa Integrated Rural Development Project (IRDP) katika Ranchi ya Ruvu na Kampuni ya National Egyptian Company for Africa Investment (NECAI) kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaogharimu Dola za Marekani milioni 50 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 111. Mradi wa ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa utaweza kuchinja ng'ombe 1,500 na mbuzi/kondoo 4,500 kwa shifti moja ya saa nane. Viwanda vingine vitakavyojengwa kwenye mnyororo mzima wa mifugo ni pamoja na Kiwanda cha Ngozi kitakachoweza kusindika ngozi hadi kupata bidhaa zake.

Pia, katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Wizara imeweka mazingira wezeshi katika ujenzi wa viwanda vya utengenezaji wa chanjo na uchakataji wa mifugo na mazao yake. Uwekezaji huo umefanywa katika miradi ifuatayo:-

Ujenzi wa jengo la kuzalishia chanjo za aina ya bakteria katika Kiwanda cha Serikali cha Kibaha (TVI). Gharama ya jengo hilo ni Sh. milioni 667. Jengo hilo linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

Ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha Hester Bioscience Africa Limited cha Kibaha. Kiwanda hicho kitazalisha chanjo 27 zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Gharama za uwekezaji wa Kiwanda hicho ni Dola za Marekani milioni 18 sawa na Sh. bilioni 41 na kinatarajiwa kuanza kuzalisha chanjo ifikapo Februari 2020.

Kiwanja cha TAN-CHOICE (Kibaha) chenye uwezo wa kuchakata ngómbe 1,000 na mbuzi/kondoo 4,500 kwa siku na uwekezaji wake ni Dola za Marekani milioni 5.5 sawa na Sh. bilioni 12.5 na kinatarajiwa kuanza kazi mwezi Septemba, 2019 pia kinatarajia kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 500.

Kiwanda cha Elia Food and Overseas Ltd (Longido) chenye uwezo wa kuchakata ng'ombe 400 na mbuzi/kondoo 2,000 kwa siku ujenzi wake ni Dola za Marekani milioni 5 sawa na Sh. bilioni 11.3 kitaanza kufanya kazi mwezi Septemba, 2019 na kinategemea kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 200.

Kiwanda cha Galaxy Food and Beverage Limited (Arusha) cha kusindika maziwa, kina uwezo wa kusindika lita 75,000 kwa siku na kimeajiri jumla ya wafanyakazi 30 kwa kuanzia. Gharama za uwekezaji wa kiwanda hicho ni Dola za Marekani milioni 2.5 sawa na Sh. bilioni 5.7. Kiwanda hicho tayari kimeshaanza kuzalisha maziwa (Kilimanjaro Fresh) kwa kiwango cha UHT tangu mwezi Machi, 2019 na

Viwanda vya nyama vya SAAFI (Rukwa), Tanganyika Parkers (Shinyanga na Mbeya) na Kiwanda cha maziwa cha Utegi na Musoma Dairy. Serikali inatafuta wawekezaji mahiri wa kuvifufua na kuviendesha viwanda hivyo.

Nane jumla ya mitamba ya ng'ombe wa maziwa 15,097 ilizalishwa na kusambazwa. Kati ya mitamba hiyo, 637 ilizalishwa katika mashamba ya Serikali na 14,460 kutoka Sekta binafsi ikilinganishwa na mitamba 13,735 iliyozalishwa na kusambazwa mwaka 2017/2018. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 2.4 mwaka 2017/2018 na kufikia lita bilioni 2.7 hadi mwezi Aprili Mwaka 2018/2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.5. Kati ya lita hizo, bilioni 1.8 zilitokana na ng'ombe wa asili na lita milioni 900 ng'ombe wa kisasa. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka 1,100,000 hadi 1,294,882.

Tisa katika mwaka 2018/2019 biashara ya mifugo imeendelea kuimarika ambapo jumla ya Sh.trilioni 1.4 zimepatikana kutokana na mauzo ya ng'ombe 2,253,100, mbuzi 2,003,200 na kondoo 385,500 ikilinganishwa na sh. trilioni 1.1 zilizopatikana mwaka 2017/2018 kutokana na mauzo ya ng'ombe 1,614,321 mbuzi 1,340,222 na kondoo 315,636 waliouzwa minadani.

Kumi, katika Mwaka 2018/2019 idadi ya mifugo inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 30.5 hadi milioni 32.2, mbuzi kutoka milioni 18.8 hadi milioni 20 na kondoo kutoka milioni 5.3 hadi milioni 5.5. Aidha, kuku wameongezeka kutoka milioni 74.8 hadi milioni 79.1 ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 38.2 hadi 38.5, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 36.6 hadi milioni 40.6, nguruwe kutoka milioni 1.9 hadi milioni 2 na punda kutoka 595,160 hadi 636,997.

Waziri Mpina pamoja na mafanikio hayo katika sekta ya mifugo, kwa namna ya pekee anawapongeza wafugaji na wavuvi kote nchini kwa kazi nzuri wanazofanya za kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa.

Mafaniko ya mengine kumi sekta ya uvuvi yataletwa katika toleo la kesho tafadhali usilikose.

***Mwandishi wa makala ni Katibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Anapatikana kwa anwani barua pepe:jmapepele1@gmail.com au simu (+255) 0784441180***



## HABARI MBEYA

# Soko la madini laingiza mil. 300/- siku 20

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SOKO la madini lililofunguliwa hivi karibuni wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, limeanza kuleta manufaa baada ya serikali kukusanya kodi ya zaidi ya shilingi milioni 300 kutokana na mauzo ya dhahabu ndani ya siku 20 tangu soko hilo lifunguliwe.

Soko hilo lilifunguliwa Mei 2, mwaka huu, kufuatia agizo ka Rais John Magufuli, alipokuwa kwenye ziara ya kikazi wilayani Chunya mwishoni mwa Aprili, ambapo aliwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuhakikisha soko hilo linafunguliwa huku akitahadharisha kuwa soko hilo ndilo jaribu la kibarua chake.

Akizungumza juzi kwenye kikao na wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya na maofisa misitu, Chalamila alisema soko hilo limeleta manufaa makubwa kwa wachimbaji na serikali kutokana na kuingiza fedha nyingi.

Alisema kilo 82 za dhahabu zimeuzwa katika soko hilo ndani ya siku 20, na kwamba uwapo wa soko hilo umeleta tija kubwa kwenye makusanyo ya kodi za serikali, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo hapakuwapo takwimu za uhakika.

"Tangu Rais ametuagiza kufungua soko, Wilaya ya Chunya pekee imeuza kilo 82 ndani ya siku chache, na kwa miaka ya nyuma kiasi hicho kilikuwa kinaonekana kinauzwa kwa mwaka au miaka kadhaa, sasa swali la kujiuliza ni kwamba maofisa madini wetu walitusaidia nini kufanya hali iwe kama ilivyo sasa?" Alihoji Chalamila.

Alisisitiza mapato ya aina hiyo yakikusanywa na kwenye vyanzo vingine ikiwamo mazao ya misitu na kilimo, serikali itakuwa na uwezo mkubwa wa kujitegemea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aliwataka wachimbaji wa dhahabu wilayani Chunya ambako ndio pekee madini hayo yanapatikana kwa Mkoa wa Mbeya, kuendelea kulitumia soko hilo pamoja na lililopo jijini Mbeya ili wanufaike zaidi na serikali ipate kodi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alisema mauzo ya dhahabu ambayo yamekwishafanyika katika soko la madini la wilaya yake ndani ya siku 20 yameinufaisha pia wilaya hiyo.

Alisema wilaya yake imeambulia mrahaba wa zaidi ya shilingi milioni 15, na matarajio yake ni soko hilo litaendelea kuwanufaisha wachimbaji pamoja na serikali.

Alisema wanaendelea na kutoa elimu kwa wachimbaji wa madini hayo ili waendelee kuuza, na kwamba hakuna mtu anayeruhusiwa kuuza madini hayo nje ya soko hilo.

Hata hivyo alisema pamoja na ugeni wa mfumo huo wa uuzaji wa dhahabu, lakini wananchi wameonyesha mwamko mzuri na kwamba ndio maana manufaa makubwa yamepatikana ndani ya siku chache tangu kuanzishwa.



Mchuuzi wa magimbi akiyatoa matope kabla ya kuwauzia wateja wake, kando ya barabara jirani na Soko la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkurugenzi amaliza mgogoro wa mil. 10/-

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

MKURUGENZI Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, amemaliza utata wa matumizi ya shilingi milioni 10 za mfuko wa jimbo zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya Shule za Msingi Nero na Mapambano zilizopo katika Kata ya Iyela kwa kutoa mchanganuo wa matumizi yake.

Kasusura alisema juzi kuwa katika mradi huo hakuna fedha iliyotafunwa kama ilivyokuwa inatafsiriwa na wajumbe wa kamati za shule hizo na kwamba wajumbe hao walikuwa wana maslahi yao binafsi. Alisema zaidi ya shilingi milioni nane zilizokuwa zimepelekwa katika Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo zilitumika kununulia vifaa na milioni moja ilitumika kumlipa fundi aliyekuwa anajenga vyoo hivyo.

Alisema fedha hizo shilingi milioni 10 zilipelekwa katika kata hiyo kwa maelekezo kuwa zigawanywe kwenye shule hizo mbili kwa kila shule kupata milioni tano ili kukamilisha mradi huo ambao ulianzishwa na baadhi ya wadau.

Alifafanua kuwa maelekezo ya fedha hizo ilikuwa kamati ya maendeleo ya kata ifanye kazi ya kununua vifaa na kuvipeleka kwenye shule hizo na wenyeviti wa mitaa wasimamie ujenzi na hakukuwa na maelezo ya fedha taslimu kupelekwa kwenye shule hizo.

"Nashangaa hizi tuhuma wanazitoa wapi, maelekezo ya zile fedha yalikuwa wazi, hawakutakiwa kupewa fedha na badala yake walikuwa wanatakiwa wapelekewe vifaa, sasa wenyewe walitaka wapewe fedha ili wawe wanapata kiasi fulani," alisema Kasusura.

Alisema baadhi ya vifaa bado vipo kwenye ofisi za shule hizo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo, na kwamba vingine vilishafanya kazi ikiwamo kuezeka vyoo hivyo. Hata hivyo, alipongeza baadhi ya wadau walioshiriki kwenye ujenzi wa vyoo hivyo vyenye matundu 16 akiwamo Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Iyela na wananchi.

# Hasunga kufungua maonyesho kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonyesho ya kilimo biashara ambayo yanafanyika kwa mara ya kwanza mkoani Mbeya kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mbinu na teknolojia bora za kilimo.

Maonyesho hayo yameandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Kituo cha Uyole kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo na yamepangwa kufanyika kwa siku mbili mfululizo.

Washiriki wa maonyesho hayo ni wakulima, kampuni za kuzalisha mbegu, wanunuzi wa mazao na wasindikaji na wazalishaji wa zana bora za kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya, Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema maonyesho hayo ni fursa nzuri kwa wakulima kujifunza teknolojia na mbinu za kilimo bora pamoja na kampuni ambazo ni wadau wa kilimo kutangaza bidhaa na teknolojia walizonazo kwa wakulima.

"Maandalizi ya maonyesho ya yamekamilika na tunatarajia Waziri wetu wa Kilimo kuwa mgeni rasmi wakati wa kuyafungua Mei 31 na kuyafunga Juni Mosi mwaka huu," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema zaidi ya kampuni kumi zimeshaandaa vipando kwenye mashamba darasa katika eneo la maonyesho kwa ajili ya kuwaonyesha wakulima namna bora ya kulima kuanzia kuandaa mashamba, kupanda, kutunza na hatimaye kuvuna.

Ofisa Programu wa Baraza la Nafaka Afrika Mashariki, Prudence Mushi, alisema kuwa maonyesho hayo yana faida kubwa kwa wadau kwa vile yatasaidia kampuni zenye teknolojia, mbinu na bidhaa za kilimo kuwafikia wakulima kirahisi.


Alisema mashamba darasa yaliyoandaliwa na kampuni mbalimbali kwenye maonyesho hayo yamezingatia mazingira halisi ya wakulima hivyo wakulima watakaofika kwenye maonyesho hayo kujifunza watanufaika kwa kujua namna ya kuendesha kilimo kwenye mazingira yao.

"Kampuni zimeandaa vipando kwenye mashamba darasa kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya wakulima kuanzia hali ya hewa, aina ya udongo na aina ya mbegu wanazohitaji wakulima, hivyo ni rahisi kwa wakulima kujifunza na kuhamishia teknolojia hizo kwenye mashamba yao na wakapata tija," alisema Mushi.

Alisema awali maonyesho hayo yalikuwa yanaandaliwa na Baraza hilo kwa kushirikiana na Tari Makao Makuu Arusha na kwamba baada ya kuona manufaa makubwa waliamua kuyahamishia Mbeya.

Aliwataka wakulima wa mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Tanzania kwa ujumla kujitokeza kwenye maonyesho hayo ili wajifunze zaidi kuhusu mbinu za kilimo na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mwakilishi wa Kampuni ya uzalishaji wa mbegu ya Seedco, Julius Ringo, alisema kuwa katika maonyesho hayo wamekwenda kuonyesha aina mbalimbali za mbegu ambazo zinaweza kutumiwa na wakulima kwa kuzingatia mazingira yao.





# Utouh ataka uwazi ripoti za CAG

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesema ripoti za ukaguzi zinazofanywa na Ofisi ya CAG zinapaswa kuwa taarifa za wazi kwa umma.

CAG huyo mstaafu alitoa kauli hiyo juzi katika mapitio ya ripoti ya CAG kwa mwaka 2017/2018 kwa wakurugenzi wa mtandao wa asasi za kiraia nchini wa kanda ya kati, katika kikao kilichofanyika jijini hapa.

Alisema ripoti hizo zinaonyesha mapato na matumizi ya fedha za bajeti zilizopitishwa na bunge ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na walipa kodi, hivyo zinatakiwa kuwa wazi.

Utouh ambaye pia Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wajibu, alisema ripoti hizo ndilo jicho la Watanzania kwenye usimamizi wa rasilimali zao kwa kuwa ndizo pekee zinazochanganua mapato na matumizi ya bajeti na utekelezaji wake.

Naye Mwenyekiti wa Mtandao wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Dodoma, Sarah Mwaga, alisema ripoti hizo zinapaswa kutolewa katika mfumo na lugha rahisi itakayowafikia wananchi wengi ili kuwajengea uelewa na kuhoji mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo yao hasa kutoka serikali kuu na serikali za mitaa.

Washiriki wa kikao hicho, Askofu Amon Kinyunyu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma na Sheikh Rashid Bura kutoka taasisi ya Kiislamu ya Dalai, walisema ofisi hiyo ndiyo muhimili wa shughuli za maendeleo na kuomba iwe huru bila kuingiliwa na mihimili mingine.

Naye Ofisa Mfawidhi Kitengo cha Kujengwa Uwezo wa Asasi kutoka Foundation for Civil Society (FCS), Nasim Losai, alisema warsha hiyo inakutanisha wakurugenzi ili kuzungumza na kutoa na fikra mbadala.

Vile vile alisema kuwa kuna ulazima kwa asasi za kiraia kuwa makini kutokana na suala la maombi ya ruzuku kuhusishwa na masuala ya rushwa.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Ave Maria Semakafu (kulia), akizungumza na ujumbe kutoka nchini China, walipotembelea ofisini kwake, jijini Dodoma juzi, kuhusu kusaidia kuingiza lugha ya Kichina kwenye vyuo vya kati nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma yaanza kuhakiki wamachinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma umeanza kuwahakiki na kuwatambua wafanyabiashara wadogo wadogo (Machinga) wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi.

Uhakiki huo ni pamoja na kutambua maeneo wanayofanyia biashara zao, majina yao kamili na aina ya biashara wanazofanya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alisema lengo ni kutofanya biashara zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kutokana na kuzagaa kila eneo. Ofisa huyo alisema uhakiki huo unafanyika kwa kushirikiana na viongozi wa wamachinga waliopo kwenye Soko la Sabasaba na lile lililopo kando kando na Viwanja vya Nyerere ambalo biashara zao hufanyika muda wa jioni.

"Kukamilika kwa uhakiki huo kwa upande wa Halmashauri ya Jiji na wafanyabiashara hao kutaondoa mahusiano yasiyo rafiki kati yao na jiji, kwa baadhi yao ambao wamekuwa na tabia ya kupanga biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi na yenye kuhatarisha maisha yao na biashara zao," alisema.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na wimbi kubwa la wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama wamachinga ambao wamekiuka sheria na kanuni za masoko waliopanga biashara holela, huku wakiacha maeneo yao waliyopangiwa ikiwamo ndani ya masoko.

"Halmashauri yetu ya jiji tuna masoko yakutosha ambayo yanaweza kutosheleza wafanyabiashara hao ambao walizagaa mitaani, ikiwamo soko kuu la Majengo, Kikuyu, Sabasaba, Chang'ombe, Makole na Chadulu, hivyo hakuna sababu ya kupanga biashara hizo katika eneo ambalo linaweza kuhatarisha maisha yao na biashara zao," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakifanya biashara zao mitaani kwenye maeneo yasiyo rasmi, walidai kuwa masoko yaliyotengwa kwa ajili yao hayatoshelezi hali ambayo inayowasababishia kukiuka sheria na kanuni zilizopo ndani ya halmashauri ya jiji.

Naye Mwenyekiti wa soko la jioni lililopo kando kando na viwanja vya Nyerere, Baraka John, alisema kutokana na adha hiyo ni wakati sasa kwa halmashauri ya jiji kutenga maeneo ya kufanya biashara kwa muda wa jioni ili wale wanaozagaa mitaani wafanye kazi zao bila kusumbuliwa.

# ESRF yatoa neno kuhusu mipango miji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na ukuaji wa kasi wa majiji nchini likiwamo jiji la Dar es Salaam, serikali imeshauriwa kuzingatia masuala ya mipango miji na upatikanaji wa huduma za kijamii kwenye maeneo hayo.

Jiji hilo linakadiriwa ifikapo mwaka 2035, litakuwa na watu milioni 10 na kwa la pili kwa Afrika kukua kwa kasi.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini hapa na Mkuu wa Kitengo cha Utafiti, Mkakati na Machapisho kutokaTaasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijami ( ESRF), Prof. Fortunata Makene, katika kikao cha kujadili rasimu ya mwongozo wa mipango miji uliowakutanisha wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wengine.

Alisema jiji hilo ni miongoni mwa majiji makubwa Afrika, hivyo kutokana na ukuaji wake wa kasi ni vyema serikali ikatambua imejiandaaje na kwenye suala la mipango miji.

"Sisi Tanzania tumejiandaaje kama jiji linakua huduma za kijamii ziweje kwenye hospitali, shule, barabara, umeme ili kukidhi matakwa ya Mtanzania wa kawaida," alisema.

Aliongeza kuwa: "Jiji linapokuwa na watu milioni 10 kutakuwa na changamoto mbalimbali kama utoaji huduma za maji, ukusanyaji na uondoaji maji safi na maji taka, lazima uangalie na kuzibainisha, kwa hiyo tumeangalia hizo changamoto ambazo miaka hiyo majiji mengi yanayokua yatakumbwa nazo."

Hata hivyo, alisema watu milioni 45 wanatarajiwa kuishi mijini nchini Tanzania ifikapo mwaka 2050, hivyo ni vyema majiji yakajiandaa kutoa huduma kwa watu hao.

Aidha, alisema ili Tanzania kufikia uchumi wa kati, huduma mbalimbali za kijamii na kimiundombinu zinatakiwa kuboreshwa na changamoto zilizopo kwenye majiji zishughulikiwe.

Prof. Makene alisema wameanza kuufanyia kazi mwongozo huo mwaka 2017 ili kufanya utafiti ambao unalenga kuisaidia Tanzania kwenye eneo la mipango miji.

"Kwa sababu sisi watafiti tuliona kuna nafasi katika serikali ya sasa kupitia mpango wa pili wa maendeleo wa taifa ambao moja ya kipaumbele ni mipango miji. Sisi watafiti tuna mchango wetu na mchango wetu ni kwenye masuala ya kisera, kwa hiyo tulianza huo mchakato kwa kufanya majaribio mbalimbali," alisema.



Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Dk. Juma Muhammed (kushoto), akibadilishana mawazo na Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaahidi marekebisho Sheria ya Utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, imesema inakusudia kuipitia Sheria ya Utalii na kuifanyia marekebisho ili kutoa nafasi kwa vijana wazalendo kuajiriwa katika miradi ya hoteli za kitalii.

Waziri wa wizara hiyo, Mahmoud Thabit Kombo, alisema hayo wakati alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za michango iliyotolewa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wa kuchangia bajeti hiyo katika kikao cha bajeti kinachoendelea visiwani hapa.

Alisema utafiti unaonyesha kwamba asilimia 60 ya wananchi wazalendo ndio walioajiriwa katika sekta ya miradi ya vitega uchumi ikiwamo hoteli za kitalii, huku lengo la serikali ni kuona kwamba sekta hiyo inatoa ajira kwa vijana wazalendo kwa asilimia 90.

"Kwa mfano sekta ya utalii inazalisha ajira moja kwa moja jumla ya wananchi 33,000, huku zikiwapo ajira ambazo sio moja kwa moja zinazowahusisha wasambazaji wa huduma za vyakula hotelini wapatao 66,000," alisema.

Akifafanua alisema zipo sababu mbalimbali ambazo zinawafanya vijana kushindwa kuajiriwa katika sekta ya uwekezaji wa miradi ya hoteli za kitalii, ikiwamo kukosa sifa na vigezo vya kuajiriwa katika nafasi za juu za uongozi ambazo zinahitajika katika masuala ya uongozi wa hoteli.

Sababu nyingine alisema baadhi ya wananchi waliopo katika miradi jirani ya hoteli za kitalii hawapo tayari kufanya kazi katika hoteli kwa sababu za mila na utamaduni na silka za wananchi.

Alizitaka taasisi zinazotoa elimu masuala ya utalii kuongeza idadi ya wahitimu ili kukidhi mahitaji ya wafanyakazi wenye sifa kuajiriwa katika hoteli hizo.

# Oman yatenga bil. 10/- kukarabati Beit-al-Jaib

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMLA ya shilingi bilioni 10 zimetengwa na Serikali ya Oman kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la maajabu ya historia ya mambo ya kale "Beit-al-Jaib" liliopo eneo la Mji Mkongwe visiwani Zanzibar.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, wakati akitoa ufafanuzi wa maendeleo ya ukarabati wa jengo hilo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujua maendeleo ya kazi hiyo.

Alisema hatua ya kwanza zilizochukuliwa ni kulilinda jengo ili lisiporomoke na sasa lipo katika hali ya usalama hususan katika kipindi hiki cha mvua za masika.

Alisema serikali inafanya hivyo ili kuona wanalirudisha jengo hilo katika uhalisia wake wa awali.

Alisema kabla ya kuanza ukarabati mkubwa lilihitaji kuzuiliwa na kuwekewa vyuma ili matengenezo madogo madogo yafanyike na jumla ya Sh. milioni 250, zilitumika ambazo zimetolewa na Serikali ya Oman.

Alizitaja hatua zinazoendelea kuchukuliwa kwa sasa ni kufunguliwa kwa zabuni ya tenda ya ujenzi wa jengo hilo kazi ambayo inatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu.

"Mheshimiwa Spika nataka kusema kwa ufupi kwamba kazi za ukarabati wa jengo la "Beit-al Jaib" unaendelea hatua kwa hatua na wala haijasimama," alisema.

Akifafanua alisema Serikali ya Oman kupitia viongozi wake mbalimbali waliotembelea Zanzibar mwaka huu wameahidi pia kulifanyia ukarabati jengo la Kasri la makao makuu ya wafalme waliopita 'People Palace' liliopo Forodhani mkabala na Bandari ya Malindi.

Alisema ukarabati huo ni muhimu ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa kutunza historia ya Zanzibar ya watawala mbalimbali waliopata nafasi ya kuongoza visiwa vya Unguja na Pemba.

# Serikali kuimarisha ulinzi kwa watalii Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imejipanga kuhakikisha ulinzi wa wageni wanaotembelea Zanzibar wakiwamo watalii unaimarishwa ili kudhibiti matukio ya uhalifu.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za (SMZ), Shamata Shaame Khamis ambaye alisema kuwa juhudi mbalimbali na mikakati imeimarishwa kwa ajili ya kuona hakuna vitendo na matukio ya uhalifu wanayofanyiwa watalii wakati wanapotembelea Zanzibar.

Khamis aliyasema hayo baada ya kuwapo kwa baadhi ya watalii wa nchi kama Israel kusitisha safari za kuitembelea Zanzibar huku wakidai hakuna usalama wa kutosha wa raia wao.

Katika juhudi hizo moja wapo ni kuwekwa kwa kamera za CCTV eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar kwa ajili ya kudhibiti matukio hayo.

Aidha, alisema doria mbalimbali zimekuwa zikifanywa katika maeneo ya hoteli za kitalii yaliopo kaskazini Unguja pamoja na kuimarisha vituo vya polisi.

"Suala la ulinzi na usalama wa watalii halina mjadala tumejipanga vizuri sana kuona kwamba matukio hayo yanadhibitiwa kwa kiwango kikubwa na zimekuwapo doria endelevu katika maeneo yote ya ukanda wa hoteli za kitalii," alisema.

Mapema Khamis aliwataka wamiliki wa miradi ya uwekezaji sekta ya utalii kutumia kampuni ya ulinzi za wakala wa JKU ambayo ipo kwa mujibu wa sheria katika masuala ya ulinzi.

Alisema tayari kampuni hiyo imekuwa ikitoa huduma za ulinzi kwa baadhi ya miradi ya uwekezaji wa hoteli za kitalii ili kusaidia kudhibiti matukio ya uhalifu na kusema kuwa hatua hizo zimechukuliwa kuhakikisha kwamba Zanzibar inapokea watalii wengi zaidi katika bara mbalimbali duniani.

# EA yatakiwa kushirikiana udhibiti wa bidhaa bandia

**Na Mary Geofrey**

NCHI za Afrika Mashariki (EA), zimeshauriwa kushirikiana kuweka mikakati ya pamoja ya kudhibiti bidhaa bandia ambazo zinaingia sokoni kwa asilimia 40.

Ushauri huo, ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Tume ya Kupambana na Bidhaa Bandia nchini Kenya (ACA), Flora Mtahi, wakati akizungumza katika mkutano wao na Tume ya Ushindani (FCC) katika ziara yao ya kujifunza nchini.

Alisema nchi moja moja haziwezi kudhibiti uingiaji wa bidhaa bandia sokoni, hali ambayo inasababisha kuendelea kuzunguka na kuendeleza kudidimiza uchumi.

"Tumekuja Tanzania kwa ajili ya kubadilishana mawazo na FCC na kuangalia namna ya kuboresha utendaji kazi wetu," alisema Mtahi na kuongeza:

Kikubwa tunachoweza kufanya kama nchi zinazoendelea katika kudhibiti uingiaji wa bidhaa zisizo na ubora sokoni ni kuunganisha nguvu ya pamoja kwa kuwa na sheria zitakazosimamiwa na kuwa na mipango ya pamoja."

Alifafanua kuwa asilimia 40 ya bidhaa bandia zinaingia sokoni katika nchi za Afrika zinasababisha kudhoofisha ukuaji wa uchumi wa nchi hizo.

Aidha, alisema kuwapo kwa bidhaa zisizo na ubora sokoni kunasababisha kufukuza wawekezaji kwenye nia ya dhati ya kutengeneza bidhaa zenye ubora.

Naye Mwenyekiti wa FCC, Humfrey Moshi, alisema wanasimamia suala la bidhaa bandia kwa kuzuia uingiaji wake kuanzia bandarini, kudhibiti kuingia dukani, kuwanyang'anya wauzaji na kuwatoza faini.

Alisema changamoto kubwa katika sekta hiyo ni uelewa mdogo kutoka kwa watumiaji wa bidhaa hizo kwa sababu ya Watanzania wengi hupenda kununua bidhaa za bei nafuu badala ya kuzingatia ubora.

Alisema kuendelea kuingia kwa bidhaa hizo kunachangia kwa kiasi kikubwa kukimbiza wawekezaji wenye nia njema na kusababisha madhara ya afya kwa watumiaji.

# DC Dar aeleza siri maeneo kutovamiwa

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, amewataka wananchi kuhakikisha wanalinda maeneo ya wazi ili yasivamiwe.

Chongolo alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam alipotembelea eneo la mgogoro wa ardhi katika eneo la Tegeta Masaiti kwa ajili ya kutoa maamuzi. Chongolo alisema ipo tabia ya uvamizi wa maeneo ya wazi ambayo serikali iliyatenga kwa ajili ya matumizi maalum na kutaja eneo la Tegeta kukithiri kwa vitendo hivyo vya uvamizi wa maeneo hayo.

Pia, alisema wapo baadhi ya watumishi wa ardhi katika miaka ya nyuma ambao hawakuwa waaminifu ambao walitumia ujanja ujanja kuwauzia wananchi maeneo ya wazi ambayo yaliachwa wazi na serikali kwa ajili ya matumizi maalum.

"Nimekuja hapa kwa lengo moja tu, kutangaza matokeo ya uchunguzi wa serikali kuhusu mgogoro wa siku nyingi katika eneo hili la kiwanja namba 444," alisema Chongoro na kuongeza:

"Kiwanja namba 444 ambacho kimesababisha mgogoro wa muda mrefu kati ya serikali, wananchi majirani pamoja na anayedaiwa kumilikishwa ni eneo la wazi na hatakiwi kumilikishwa mtu wa aina yoyote. Kuna mchezo ambao ulifanywa na baadhi ya maofisa ardhi wasio waaminifu ambao walichezea namba za viwanja hivi wakamuuzia mwananchi kiwanja ambacho hakipo, halafu yeye anasema aliuliziwa kiwanja hiki namba 444 ambalo ni eneo la wazi, hili ni mali ya wananchi na halitakiwi kuguswa."

Willy Kusaga, anayedaiwa kumilikishwa eneo hilo, alisema hakubaliani na maamuzi yaliyochukuliwa na Mkuu wa Wilaya na kutangaza kukata rufani ili serikali impatie eneo lake.

"Sijakubaliana kabisa na maamuzi ya Mkuu wa Wilaya, mimi nina 'document' (nyaraka) zote za manunuzi ya kiwanja hiki namba 444, kama watumishi wenyewe ndiyo waliojichanganya basi wao ndio walaumiwe na siyo kunyang`anya haki yangu, ni lazima nikate rufani," alisema Kusaga na kuongeza:

"Nilitegemea kwamba serikali kwa sababu imefahamu makosa yaliyofanywa na watumishi wake ingedili na watu wake na au la inipatie eneo langu jingine, lakini kwa sababu imeninyang`anya na haijasema lolote kuhusu haki yangu, lazima nitafute haki mahakamani."



Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya Exim Tanzania, Andrew Lyimo (kulia), akizungumza na wateja wa benki hiyo waliohudhuria hafla ya futari iliyoandaliwa kwa ajili ya wateja wa huduma za reja reja wa benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Maabara za kupima udongo kuboreshwa

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, amesema serikali itaboresha maabara za kupima udongo nchini na kuhakikisha zinafanya kazi kikamilifu ili kuwa na kilimo chenye tija.

Bashungwa alitoa ahadi hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wakulima wa kilimo cha umwagiliaji nchini, katika mkutano wa wadau wa kilimo, uliondaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi ya Kilimo cha Mboga (Taha).

"Natambua changamoto ya upimaji wa udongo katika maabara nchini, serikali inafanyia kazi suala hili na kuhakikisha tunakuwa na maabara za kisasa zinazotoa huduma kwa ajili ya kuwa na kilimo chenye tija," alisema Bashungwa.

Alisema pia changamoto ya kuwapo na uhaba wa mikopo kwa wakulima, hali inayosababisha sekta hiyo kukwamisha wanaifanyia kazi kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini.

Alisema wataisaidia Taha kufikia fursa hiyo ili kuzalisha wakulima wengi zaidi ambao watasaidia kukuza sekta hiyo na uchumi wa Taifa pia.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taha, Jacquiline Mkindi, alisema lengo la mkutano huo ni kuwajengea uwezo wadau wa kilimo kuzalisha mazao yanayokidhi soko la kimataifa.

Alisema lengo la sekta binafsi ni kuongeza mtaji wa kilimo cha mazao yanayouzwa nje ya nchi kutoka Dola za Marekani milioni 700 kwa sasa hadi kufika Dola bilioni mbili kwa mwaka.

Alisema changamoto kubwa zinazowakabili sekta hiyo ni mabadiliko ya tabianchi, mvua kuchelewa, joto linalozidi na magonjwa mapya likiwamo la mnyauko.

"Magonjwa ya mnyauko yamesababisha mazao mengi kuharibikia shambani na sababu kubwa inatokana na kutokuwapo na maabara za kusasa zenye vifaa vya kupima udongo hali inayotula-

HABARI KIMATAIFA

## Maofisa Kenya waenda kufuatilia dhahabu bandia

**NAIROBI,** Kenya

MAOFISA wa idara ya ujasusi nchini Kenya, wameenda Dubai ili kuchukuwa taarifa ya mwakilishi wa Umoja wa Falme za Kiarabu kuhusiana na sakata la dhahabu bandia linalochunguzwa.

Wakati huohuo, kunaripotiwa kuwa katika bunge la nchi hiyo wabunge wako katika mchakato wa kukusanya saini ili kumtimua waziri wa usalama, Fred Matiangi, kwa madai ya kuwalinda watuhumiwa wa kashfa hiyo.

Polisi nao wamesema kuwa maafisa wao waliokuwapo kwenye eneo ilikopatikana dhahabu hiyo bandia ambao walikuwa wanawalinda wanadiplomasia na wala sio wahalifu.

Maofisa wa idara ya ujasusi wa Kenya walitazamiwa kusafiri juzi jioni kuelekea Dubai ili kuchukuwa taarifa ya mwakilishi wa Umoja wa Falme za Kiarabu kuhusu sakata hilo la dhahabu bandia linalochunguzwa.

Majasusi hao wanatazamiwa kumhoji Ali Zandi anayemuwakilisha Sheikh Mohammed bin Rashid Al Maktoum na kampuni ya Zlivia inayofanya biashara ya dhahabu Dubai. **DW**

## Kundi la IS 'lapiga kambi' Congo

**KINSHASA,** Congo

WAKUU wa vyombo vya usalama katika kanda ya Maziwa Makuu, wanakutana nchini Uganda kupanga mikakati ya kukabiliana na tishio la kundi la Islamic State, ambalo linasemekana limeanza kuendesha harakati zake katika maeneo ya Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kuna uwezekano wa eneo hilo kuingiliwa kirahisi na wanamgambo wa kundi hilo kutokana na ukosefu wa usalama na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola ambao unatatiza juhudi za kukabiliana nao. Vyombo vya usalama katika eneo hilo sasa vinataka kuhakikisha kuwa kundi hilo halipati nafasi kuendesha shughuli zake katika matatifa ya eneo hilo baada ya kutimuliwa mashariki ya kati.

"Kuna vitisho kwa hivyo ni onyo kwetu kulishughulika mapema kabla halijawa tatizo kubwa katika kanda ya maziwa makuu" alisema Mkuu wa Jeshi la Uganda, Jenerali David Muhoozi'

Kulingana na wakuu hao wa usalama walikubaliana kuwa kuna haja ya wao kushirikiana na majeshi ya mataifa ya kigeni yaliyochangia katika juhudi za kuvunja kundi hilo mashariki ya kati.

"Tishio la kundi hilo la kigaidi ni kubwa kiasi ya kuhamasisha Serikali za eneo hili lote la Maziwa Makuu, kuona ya kwamba zinaongeza juhudi za kukabiliana masuala ya kigaidi iwe ni kutoka kwa kundi la al-Shabab, ISIS, Boko Haram au Al-Qaeda", alisema katibu mtendaji wa mataifa ya maziwa makuu, Zachary Muburi Muita. **BBC**

# Mataifa Ulaya yataka maafikiano Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MAREKANI, Uingereza na Norway zimeitaka Sudan kuhakikisha inapata makubaliano ya haraka kati ya waandamanaji na viongozi wa kijeshi, kuhusu kuundwa serikali ya kiraia.

Mazungumzo baina ya viongozi wa waandamanaji na wanajeshi waliochukua mamlaka baada ya kiongozi wa muda mrefu Omar al-Bashir kuondolewa madarakani yalikwama tangu Jumatatu jioni kufuatia kutoelewana juu ya nani ataongoza serikali.

Mataifa hayo ya Ulaya ambayo awali yalihusika na mazungumzo ya upatanishi katika migogoro ya Sudan, yamesema nchi hiyo inahitaji makubaliano ya haraka ili kumaliza kipindi cha hali ya sintofahamu, kwa mujibu wa taarifa ya pamoja iliyotolewa siku ya Jumanne.

Lakini wananchi wamekuwa na maoni tofauti kuhusiana na mkwamo uliopo nchini humo.

Mmoja wa waandamanaji, Abu Baker Abdullah alisema ni muhimu kwa wasudan wote kuzidisha uasi wa kiraia.

**Watu wa Sudan lazima watoke kama walivyofanya Aprili 6 ili kuweka shinikizo zaidi kwa baraza la kijeshi ili kutupatia sisi mamlaka kamili.**

"Watu wa Sudan lazima watoke kama walivyofanya Aprili 6 ili kuweka shinikizo zaidi kwa baraza la kijeshi ili kutupatia sisi mamlaka kamili," alisema Abdullah.

Taarifa ya mataifa hayo zinaeleza kuwa uamuzi wowote ambao utakwamisha kuundwa serikali itakayoongozwa na raia, haitakuwa imetimiza matakwa yaliyowekwa wazi na watu wa Sudan ya kutaka utawala wa kiraia.

Marekani mara kadhaa imesisitiza juu ya utawala wa kiraia nchini Sudan tangu Rais Bashir aondolewe na jeshi Aprili 11, baada ya miezi kadhaa ya maandamano ya nchi nzima dhidi ya utawala wake wa miaka 30.

Pia imeahirisha mazungumzo na Khartoum kwa ajili ya kuiondoa Sudan katika orodha ya nchi zinazofadhili ugaidi.

Hiyo ilikuwa sababu muhimu kwa Marekani ambayo kwa miongo kadhaa imekuwa ikitia wasiwasi uwekezaji wa kigeni katika taifa hilo la Kaskazini mashariki mwa Afrika.

Viongozi wa waandamanaji nchini Sudan hivi sasa wanaandaa mipango ya maandamano makubwa kwa ajili ya kuwashinikiza zaidi majenarali wa kijeshi ili waachie madaraka.

Baraza la kijeshi linalotawala nchini Sudan limekuwa likihimiza kuwa mwenyekiti wake Jenerali Abdel Fattah al-Burhan aongoze serikali mpya, jambo linalogomewa na viongozi wa waandamanaji wanaotaka kiongozi wa kiraia.

Iwapo chombo kipya cha utawala kitakapokamilika kinatarajiwa kuanzisha serikali ya kiraia ya mpito kwa miaka mitatu na baadae kufanya uchaguzi wa kwanza baada ya Rais Bashir kuondolewa. **DW**



Mzee katika mji wa Blantyre nchini Malawi, akipiga kura kumchagua rais mpya wa nchi hiyo. **PICHA: AP**

# Mutharika, Chakwera watoana jasho

**LILONGWE,** Malawi

MATOKEO ya awali ya urais nchini Malawi yanaonesha kuwa kuna ushindani mkali kati ya Rais Peter Mutharika na mgombea wa upinzani, Lazarus Chakwera.

Hata hivyo, Chakwera anaonekana kuwa mbele kwa karibu kura elfu 10, wakati zoezi la kuhesabu kura likiendelea kujumuishwa na maafisa wa Tume ya Uchaguzi.

Chakwera anaongoza kwa kura 533,000, huku Rais Mutharika akiwa na kura 524,000.

Hata hivyo, Chakwera ameonya kuwa kuna uwezekano wa kutokea kwa wizi wa kura, wakati huu Tume ya Uchaguzi ikitarajiwa kutangaza matokeo ya mwisho muda wowote.

Akiwa mjini Blantyre Chakwera alisema chama chake cha Malawi Congress Party (MCP) kinafanya mahesabu yake na kina uhakika wa kupata ushindi.

"Hadi sasa ujumbe upo wazi, tunajua kuwa tunaongoza, Hakuna anayekwenda kuiba uchaguzi huu. Haki itatendeka," " alisema Chakwera.

Waangalizi wa Uchaguzi wanasema zoezi hilo la upigaji kura lilifanyika kwa amani na utulivu. **RFI**

# Wasomi: Mfumo wa elimu ufumuliwe

**Na Beatrice Moses**

WASOMI kadhaa wanatamani mfumo wa elimu ufumuliwe ili usukwe upya kwa lengo la kuwezesha kupatikana wahitimu wengi wenye uwezo wa kujiajiri na wenye kuleta ushindani katika soko la ajira.

Wakichangia kuhusu mfumo wa elimu nchini na Afrika wakati wa mjadala kwenye Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere jijini Dar ers Salaam jana, walibainisha elimu inayotolewa sasa haikidhi mahitaji yaliyopo hivyo kusababisha pengo, hasa kwenye sekta ya ajira.

Dk. Evalisto Mtitu Mhadhiri wa Elimu kutoka Chuo Kikuu Huria (OUT), alisema mjadala huu unatusaidia kupata namna nzuri ya kuboresha elimu nchini na Afrika kwa ujumla.

Alisema katika Karne ya 21 kama wanataaluma wanapaswa kuwaandaa wanafunzi ili waweze kujitegemee na kuendeleza ile falsafa ya Mwalimu ya kuunganisha nadharia na vitendo kuwezesha anayepata elimu aweze kujitegemea katika kujitafutia kipato.

"Aina ya ufundishaji uliopo wanafunzi wanafundishwa kwa mbinu za zamani ya nadharia zaidi ambayo haiwezi kusaidia wakihitimu waweze kujiajiri, ufundishaji unaolenga zaidi mitihani lakini siyo vitendo," alisema Dk. Mtitu.

Alisema hali hiyo imechangia uwepo wa vijana wengi wahitimu mtaani. "Mwanafunzi anapata elimu ya kujibu mitihani yaani wafaulu kwa alama za juu na siyo kuwa na mbinu za kuyakabili maisha, hivyo atakumbuka ili kukidhi matakwa ya walimu au taifa anapopimwa kwenye mitihani ya taifa," alisema.

Mkurugenzi wa Haki Elimu, John Kallaghe, alisema mfumo wa elimu nchini haukidhi kwani hatujawafanya wahitimu kuweza kuanzisha vyanzo vya mapato au kushindana kwenye soko la ajira.

"Ili kupata maendeleo suala la elimu ni ufunguo mada zilizowasilishwa mfumo wa elimu haulingani na mahitaji ya sasa hivyo kuna umuhimu wa kuwa na mjadala mpana kuhusu jambo hili," alisema.

"Tunapaswa kuangalia tatizo kubwa lipo wapi namna gani tunaweza kutoka hapo, tuchukue hatua za kuboresha mfumo wetu wa elimu, hivyo mjadala huu ni sehemu ya mjadala tunaoutaka wa kitaifa kuhusu namna gani elimu inayotolewa iweze kwenda na matakwa ya sasa," alisema Kallaghe.

Alisema mwisho kuna mapendekezo yatatolewa ambayo yanaweza kutoa mchango katika kutafuta suluhisho kwa jambo hili. Majadiliano yanalenga kuangalia elimu ngazi yote. Msingi, sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya ufundi.

Mhadhiri wa Saikolojia ya Elimu na Taaluma za mitaala kutoka Chuo cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), DK. Florence Kyaruzi, alisema inabidi tufanye tathmini ingawa naona tupo katika hatua za kuboresha tunapata changamoto na pia tunapata mrejesho.

Ilibainishwa kuwa kuna watoto milioni 3,500,000 hawapo kwenye mfumo wa elimu badala yake wamekuwa wakitumika katika kazi mbalimbali kwenye mashamba na migodini.

Dk. Abdallah Hamza wa UDSM, alibainisha kuwa kuna tatizo la baadhi ya jamii kutoona umuhimu wa elimu kwa watoto, katika utafiti uliofanywa Ilula ulibaini kuwa watoto wenye umri wa kati ya miaka 6 hadi 17 wanafanya kazi kwenye mashamba.

Alisema asilimia 81 ya wazazi wanakubaliana na hali hiyo ambayo ilibainisha pia eneo la Buhemba utafiti ulibaini watoto wameajiriwa kwenye kampuni kubwa na ndogo za migodi kinyume na sheria za nchi, ambapo haziruhusu ajira kwa watoto.

Awali Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Prof. Rwekaza Mukandala, alisema katika tamasha hilo pamoja na mijadala ya mada, nyinginezo pia wamekusudia kujadili nafasi ya elimu na ubora wa elimu na jinsi gani inaweza kuleta maendeleo.



Meneja Mawasiliano wa Zantel, Rukia Mtingwa (katikati), akiwasajili wabunge kwa alama za vidole kwa ajili ya laini zao za simu baada ya kufika katika banda la kampuni hiyo, katika Viwanja vya Bunge jijini Dodoma hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu wa kidato sita sasa watakiwa kuripoti JKT Juni 1

**Na Gwamaka Alipipi**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limewataka wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2019, waripoti katika kambi walizopangiwa kuanzia Juni mosi hadi saba.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Habari na Uhusiano, Makao Makuu ya JKT, ilieleza wanafunzi hao ni kutoka shule zote za Tanzania Bara ambao wanatakiwa kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria.

"Jeshi la Kujenga Taifa limechagua vijana waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2019 kutoka shule za Tanzania Bara, sambamba na uchaguzi huo, JKT imewapangia kambi watakazokwenda kupatiwa mafunzo kwa miezi mitatu," ilieleza taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa vijana waliochaguliwa wamepangiwa katika kambi za JKT Rwamkoma-Mara, JKT Msange-Tabora, JKT Ruvu-Pwani, JKT Mpwapwa na JKT Makutupora-Dodoma, JKT Mafinga-Iringa, JKT Mlale-Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba-Tanga.

Kambi zingine ni JKT-Makuyuni-Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa, JKT Mtabila-Kigoma, JKT Itaka-Songwe, JKT Lua na JKT-Milundikwa-Rukwa, JKT Nachingwea-Lindi.

Kadhalika, ilieleza kuwa wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho wanatakiwa kuripoti kambi ya JKT-Ruvu iliyopo Mlandizi mkoani Pwani ambayo ina miundombinu ya kuhudumia watu wa jamii hiyo.

Ilieleza kuwa orodha kamili ya majina ya vijana waliochaguliwa, maeneo ya makambi ya JKT waliyopangiwa na vifaa wanavyotakwa kwenda navyo inapatikana katika tovuti ya HYPERLINK "http://www.jkt.go.tz" \t "_blank" www.jkt.go.tz .

# Binti adaiwa kuunguzwa kwa maji na mama kambo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BINTI mwenye umri wa miaka 16 (jina limehifadhiwa), mwanafunzi wa darasa la saba Shule ya msingi Kashenge iliyoko katika Manispaa ya Bukoba, amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera akiuguza majeraha anayodai kuyapata baada ya kuunguzwa kwa maji ya moto na mama yake wa kambo.

Akizungumza kwa shida katika wodi namba kumi iliyoko katika hospitali hiyo, binti huyo alisema mama yake alifika nyumbani na kumkuta amepika viazi akamuuliza kwa nini alipika viazi bila kuambiwa, ndipo akammwagia maji ya moto.

"Baada ya kuingia jikoni akakuta nimepika viazi alichukua sufuria na kunimwagia, niliamua kuondoka na kuingia ndani, akaja mdogo wangu akaniambia twende kwa mtendaji tukaenda hatujamkuta," alisema.

Binti huyo alisema mama yao mzazi alitengana na baba yao na kuwaacha wakiwa watano yeye na wadogo zake wanne.

Ofisa muuguzi msaidizi wa wodi namba kumi upande wa upasuaji, Edith Ezekiel, alisema walimpokea binti huyo juzi akiwa ameunguzwa mkono wa kulia, titi na sehemu za bega, na kuwa hali yake inaendelea vizuri.

Mama mzazi wa binti huyo aliyefahamika kwa jina la Alodia au mama Judith, alisema akiwa nyumbani kwake wilayani Muleba alipata taarifa kwa njia ya simu kutoka kwa jirani na wanakoishi watoto hao, na kumwambia mtoto wake ameunguzwa kwa maji ya moto.

"Nilipopata taarifa hizo nikafika kwa ajili ya kumuona nikakuta kweli ameunguzwa," alisema.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema atatoa taarifa rasmi leo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

### NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836


**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACE BOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


### KUPOTEA KWA CHETI



**Ambroce A. C Moyo** anatangaza kupotelewa na cheti GCE chenye namba U001/0533 na chuo cha DIT mwaka 1994. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa: **DAR/MBA/RB/2312/2019**

115245102


### KUPOTEA KWA CHETI



**Lorna Mndewa** anatangaza kupotelewa na cheti cha diploma chenye namba ya **174/DPS/T/2013** kilichotolewa na chuo cha Ruaha Catholic University mwaka 2016. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/14669/2019**

115244802

### KUPOTEA KWA CHETI



**NEBO S. KASWEMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX NAMBA S.3937-0027** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA TAIFA MWAKA 2016 KATIKA SHULE YA SEKONDARI SUMA, YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **SMT/RB/6040/2019.**

115246002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA KUMBUKUMBU NA. 12 YA 2009**

**TANZANIA FERTILIZER COMPANY LTD ......... MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **RUVUMA EXPORTS COMPANY (T) LTD**
2. **STANDARD COMMERCIAL TOBACCO........WAJIBU MAOMBI SERVICE (T) LTD (STANCOM)**

---

**KWA:**
1. **RUVUMA EXPORTS COMPANY (T) LTD**
2. **STANDARD COMMERCIAL TOBACCO SERVICE (T) LTD (STANCOM)**

**POPOTE WALIPO.**

Mnajulishwa kwamba Shauri la Maombi ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 4/6/2019 saatatukasoroboasubuhi (2:45).

Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria basi maombi hayo yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo hii tarehe 16/5/2019

115244702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WENXIONG HONG**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA TOYOTA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.825 CVZ** RANGI YA SILVER CHASSIS NAMBA **AZR650110661** ENGINE NAMBA **1AZ5092771**.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MB/TR/RB/692/2019.**

115245902

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GUOYIN WANG**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TRUCK YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.356 DCU** RANGI NYEUPE CHASSIS NAMBA **LFNA7LCA2EAC12627** ENGINE NAMBA **70034983.**YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MB/TR/RB/692/2019.**

115245802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi**

**Ombi la MESHACK ELIYA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu MOLENI SUDAYI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 30/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huy upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 17/5/2019

215244452

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**JEMA B. KIMOLO**
anatangaza kupotelewa na kadi ya BAJAJI i aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC28.** Chassis namba **MD6M14PK9D4K20516.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KON/RB/926/2019.**

215244602


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DESCHAMPS: NIPO TAYARI KUMPELEKA POGBA REAL

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amesema kuwa yupo tayari kumsaidia kiungo wa Manchester United, Paul Pogba katika mpango wake wa kutaka kujiunga na Real Madrid.

Pogba kwa muda sasa amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua pale Real Madrid na anatajwa kwamba anaweza kuhamia pale kipindi hiki cha majira ya joto.

Pogba ambaye Deschamps amemtaja kwenye kikosi chake cha Ufaransa kitakachocheza mechi mbili za kufuzu Euro 2020, amekuwa akihusishwa na mpango huo wa kutimkia Bernabeu.

Siku za karibuni Pogba amekuwa akicheza chini ya kiwango, lakini jambo hilo halijawahi kuwa tatizo kwa Deschamps na kuamua kumjumuisha katika kikosi chake cha kwanza kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Bolivia halafu itafuatia mchezo wa kufuzu Fainali za Euro 2020 dhidi ya Uturuki na Andorra mwezi ujao.

Deschamps alisema: "Kushuka kiwango si kitu cha Paul peke yake. Kama ataniuliza kuhusu kuhamia Real Madrid, basi nitampa ushauri wangu."

Kocha Deschamps ameendelea kuwa na imani kwa Pogba licha ya kuwapiga chini straika wa Alexandre Lacazette, beki wa Manchester City, Aymeric Laporte na mshambuliaji wa United, Anthony Martial.

# De Gea sasa kutua PSG



**MANCHESTER,** England

SASA ni wazi kuwa mambo yamekuwa ni moto pale Manchester United, baada ya golikipa wake namba moja, David de Gea kubainisha kwamba, ataondoka katika klabu hiyo kipindi hiki cha majira ya joto.

Kipa huyo amekuwa katika kiwango cha juu na kuisaidia Manchester United katika michezo yake mingi ya Ligi Kuu England msimu uliomalizika.

Manchester United ipo katika presha kubwa ya kumuuza kipa wake huyo baada ya 'kukataa dau la mwisho alilopewa' huku Paris Saint-Germain ikiwa tayari kumsajili kwa pauni milioni 60.

Mabingwa wa Ufaransa, PSG wapo tayari kumlipa De Gea kiasi cha mshahara anachotaka cha pauni 350,000 kwa wiki huku wakiweka wazi wapo tayari kutoa dau la pauni milioni 60 alizohitaji ili kumsajili msimu huu.

De Gea ameshinda tuzo ya Kipa Bora wa Ligi Kuu England katika misimu mitano kati ya saba, huku ndani ya United ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora kwa misimu minne mfululizo kati ya 2014 and 2018.

Vyanzo vya ndani vya mtandao wa The sun, vimebaini kuwa kipa huyo, anadaiwa kuweka wazi kwamba hayupo tayari kuendelea kusalia Old Trafford msimu ujao wa 2019/20.

# *Inter kuwasajili Lukaku, Moses*


**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan inataka kuwasajili, Romelu Lukaku na Victor Moses kipindi hiki cha majira ya joto, mara tu wakimteua Antonio Conte kuwa kocha mpya, Sky Sports imebainisha.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea anatarajiwa kuchukua nafasi ya Luciano Spalletti pale Inter wiki ijayo, kwa mujibu wa Sky Sports Italia na wachezaji wote wawili wapo kwenye rada zake.

Conte alijaribu kumsajili Lukaku kipindi cha majira ya joto mwaka 2017 wakati bado akiwa pale Stamford Bridge, lakini mshambuliaji huyo aliamua kuhamia Manchester United akitokea Everton.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amefunga mabao 42 katika mechi 96 alizoichezea United, lakini alishindwa kufunga katika mechi zake nane zilizopita kwenye kipindi cha pili cha msimu huu na kumfanya Marcus Rashford kuwa chaguo la kwanza la kuongoza safu ya ushambuliaji chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.



HABARI MICHEZO

# Man United waamua kuachana na Sancho

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itaangalia uwezekano wa kufanya usajili mwishoni katika safu yao ya ushambuliaji baada ya kupiga chini mpango wa kumsajili winga, Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund.

United imeamua kuachana na mpango wa kumsajili winga huyo baada ya ada iliyotajwa ya kumnunua mchezaji huyo kuwa ni pauni milioni 80.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City, Sancho, mwenye umri wa miaka 19, kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na United huku klabu hiyo ikipigania kukijenga upya kikosi chake chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer ambaye alitua hapo kuchukua mikoba ya Jose Mourinho aliyetimuliwa Desemba mwaka jana.

Lakini wakati msaidizi wa Solskjaer, Mike Phelan alikuwa akihimiza kusajiliwa kwa kinda huyo ambaye aliichezea Timu ya Taifa ya England kwa mara ya kwanza dhidi ya Croatia Oktoba mwaka jana, United imeshindwa kufikia bei iliyotajwa kwa ajili ya mchezaji huyo na klabu yake ya Dortmund.

Kiasi hicho cha fedha kilichotajwa kwa ajili ya kuuzwa kwa Sancho, United wanakiona ni kikubwa zadi na hivyo sasa wataangalia njia mbadala ya kusamjili mchezaji mwingine kwa ajili ya kuziba pengo lake.

Mipango ya United kwa sasa imegeukia kwa winga wa Swansea City, Daniel James na kiungo wa Newcastle United, Sean Longstaff.

United pia inatajwa kuwa kwenye mipango ya kutaka kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez.






# SARRI: NIPO TAYARI KUONDOKA CHELSEA

**LONDON,** England

MAURIZIO Sarri amesema kuwa anaweza kuondoka Chelsea kama klabu hiyo ambayo itategemea majaliwa yake baada ya fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Chelsea itacheza na Arsenal kwenye fainali ya michuano hiyo mjini Baku Jumatano ijayo na tayari wamejihakikishia kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao baada ya kumaliza Ligi Kuu wakiwa nafasi ya tatu.

Lakini majaliwa ya Sarri kuendelea kuinoa timu hiyo yamebakia kuwa kwenye sitofahamu na kwamba msimu huu unaweza kuwa wa mwisho wake hapo Stamford Bridge.

Vyanzo kadhaa vimeidokeza ESPN FC kwamba Chelsea hawana mpango wa kumfukuza Sarri hata kama watashindwa kutwaa taji lolote msimu huu na kocha huyo raia wa Italia anaamini alitakiwa kuhukumiwa kwa kuangalia matokeo ya msimu wote.

Alipoulizwa kama Chelsea ikiamua kumtimua kama akifungwa kwenye fainali ya Kombe la Europa, Sarri alijibu: "Kama hali ni hiyo nataka kuondoka haraka iwezekanavyo.

Sarri alibainisha kwamba alizungumza na mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya klabu ya New England Revolution wiki iliyopita, lakini ilikuwa ni kwa dakika moja tu.

# *Bayern yajiandaa kumnasa Sane*

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich ina uhakika wa kumnasa winga, Leroy Sane kutokana na kuwa na uhusiano mzuri na Pep Guardiola ambaye ni kocha wao wa zamani wa timu hiyo

Bayern imeingiza kwenye mipango ya kutaka kuinasa saini ya winga huyo wa Manchester City, Sane ambaye ana umri wa miaka 23 ili kumrudisha nyumbani nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani katika dirisha hili kubwa la uhamisho wa wachezaji kipindi cha majira ya joto.

Sane amepoteza nafasi katika kikosi cha Guardiola na mara nyingi amekuwa akitokea katika benchi na mazungumzo mpya ya mkataba baina yake na City yamekwama huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwaka 2021.

Hata hivyo, City haitamuachia kwa urahisi staa huyo iliyemnunua kwa dau la pauni milioni 37 katika dirisha la uhamisho la mwaka 2016 akitokea Schalke 04 na itataka kiasi cha Euro milioni 100.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FIFA YASITISHA KUONGEZA TIMU 48 KOMBE LA DUNIA

## Ni baada ya kuona uamuzi mgumu kutekelezeka...

**ZURICH,** Uswisi

SHIRIKISHO la soka duniani (Fifa), limesitisha uamuzi wa kuongeza nchi zitakazoshiriki Kombe la Dunia mwaka 2022 hadi kufikia timu 48.

**Rais wa Fifa, Gianni Infantino mwaka jana alisema mpango wa kuongeza timu hizo kutoka 32 ambao ungelianza kutekelezwa mwaka 2026 urudishwe nyuma hadi mwaka 2022.**

Mabadiliko hayo yalimaanisha Qatar ambayo ndio mwenyeji wa mashindano hayo kwa kushirikiana na mataifa mengine katika kanda hiyo.

Shirikisho hilo lilisema "baada ya mashauriano ya kina" tumeonelea mabadiliko hayo "hayawezi kutekelezwa kama ilivyopangwa awali."

Fifa pia imesema ilitathmini uwezekano wa Qatar kuandaa peke yake mashindano hayo ikiwa na timu 48, lakini ikaamua kusitisha mpango huo kutokana na changamoto ya ukosefu wa muda wa kutosha wa "kufanya ukaguzi wa kubaini athari ya hatua hiyo.

Taarifa ya waandaaji wa Kombe la Dunia nchini Qatar ilisema: "Qatar ilikuwa tayari kutekeleza mpango huo katika mashindano ya mwaka 2022 na hatua iliyokua imefikia kufanikisha mpango huo ilikuwa imeafikiwa na wadau wote.

Infantino mwenye umri wa miaka 46, ambaye alirithi urais kutoka kwa raia mwenzake wa Uswisi, Sepp Blatter Februari mwaka 2016, alifanya kampeni akiahidi kupanua michuano hiyo.

Awali alipendekeza michuano ya timu 40, wazo lililowasilishwa na rais wa wakati huo wa Uefa, Michel Platini mwaka 2013, kabla ya kubadilisha msimamo na kuunga mkono michuano ya timu 48.

"Huku zikiwa zimesalia miaka mitatu na nusu kuelekea mashindano hayo, Qatar imejitolea kuhakikisha inaandaa Kombe la Dunia la mwaka 2022 ambalo litaifanya eneo zima la Uarabuni kujivunia."

Novemba mwaka jana, rais wa Uefa, Aleksander Ceferin alisema kuongeza timu 16 katika mashindano hayo ya Qatar 2022 huenda "ingelileta matatizo" na kuongeza kuwa mpango huo"hauwezekani".

Wale walio karibu na waandaaji wa mashindano hayo ya Qatar 2022 wanasema uamuzi wa pamoja ulikua umefikiwa kati yao na Fifa, lakini sasa wameamua kuangazia timu 32 zitakazoshiriki.

## ZISIKUPITE

### ROMERO KUMRITHI DE GEA

GOLIKIPA raia wa Argentina, Sergio Romero (32), anatarajiwa kupandishwa na kuwa mlinda mlango chaguo la kwanza la Manchester United kama Mhispania David De Gea ataamua kuondoka katika kipindi cha majira ya joto, kuliko klabu hiyo ya Old Trafford kutumia kiasi kikubwa cha fedha ili kuziba pengo hilo. ***(Mail)***

### RAMSEY SAFARI IMEIVA

MKUU wa Idara ya Soka wa Arsenal, Raul Sanllehi, amesema kuwa klabu hiyo itamruhusu kiungo wa Wales, Aaron Ramsey (28), kuondoka hapo kama mchezaji huru na kujiunga na Juventus ili kuweka uwiano wa mishahara na pia kulinda maslahi ya timu hiyo. ***(Telegraph, via Arsenal website)***

### TERRY ATAKIWA VILLA

NAHODHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England na Chelsea, John Terry, ambaye sasa ni Kocha Msaidizi wa Aston Villa, yuko katika mazungumzo na Middlesbrough kutua klabuni hapo kama kocha mpya. ***(Talksport)***

### CANCELO ANUKIA CITY

MANCHESTER City iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo (24), ambaye klabu yake ya Juventus imetaja thamani yake kuwa ni pauni milioni 52.9. ***(Record - in Portuguese)***

### TRIPPER AGOMBEWA

KLABU za Atletico Madrid na Napoli zimeweka wazi nia yake ya kumwania beki wa kulia wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Kieran Tripper ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

### LONGSTAFF KITAELEWEKA

NEWCASTLE United inatarajia kumpa mkataba mpya kiungo, Sean Longstaff, ambaye anahusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester United. Mkataba huo mpya utamfanya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 21 na raia wa England aendelee kubakia klabuni hapo. ***(Star)***

### DONNARUMMA KUTUA UTD

MANCHESTER United inajiandaa kumsajili golikipa wa AC Milan Mtaliano Gianluigi Donnarumma (20), kutokana na kutofahamu hatima ya Mhispania David de Gea (28) kama ataendelea kubakia Old Trafford. ***(Calciomercato, via Express)***

### BENTEKE AMFUATA FELLAINI

STRAIKA wa Crystal Palace, Christian Benteke (28), anatarajia kuungana na mchezaji mwenzake wa zamani, Mbelgiji Marouane Fellaini katika kikosi cha Shandong Luneng Taishan baada ya klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu China kukubali kutoa dau la pauni milioni 15 ili kumsajili mchezaji huyo. ***(Times - subscription required)***

### SPURS YAMNASA CLARKE

MABOSI wa Tottenham wameridhia kutoa dau la pauni milioni 10 ili kukamilisha usajili wa winga wa Leeds United, Jack Clarke, raia wa England, ambaye ana umri wa miaka 18. ***(Mail)***

### STROOTMAN SOKONI

EVERTON, West Ham na Manchester United zimepewa nafasi ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi na Marseille, Kevin Strootman (29). ***(Sky Sports)***

## KMKM kusajili wanne wapya

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Zanzibar "mabaharia" wa KMKM wanatarajia kusajili wachezaji wanne wapya kwa lengo la kukiongezea nguvu kikosi chao ambacho mwakani kitashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungunmza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu, alisema ili kukiimarisha kikosi chao kwa ajili ya msimu mpya, wamepanga kusajili washambuliaji wawili, kiungo mmoja pamoja na beki mmoja.

Msimu alisema amekusudia kusajili nafasi hizo kutokana na changamoto waliyoibaini katika msimu uliomalizika na hivyo wanataka kuona wanalimaliza tatizo hilo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar na mashindano hayo ya kimataifa.

Hata hivyo, kocha huyo hakuwa tayari kuweka wazi wachezaji hao watakaowasajili watatokea timu gani bali alisema wataangalia vigezo walivyonavyo nyota husika kabla ya kuingia nao mikataba ya kuitumikia timu hiyo.

"Siwezi kuweka wazi kwa hivi sasa kama nitamsajili nani na anatokea timu gani, muda utakapofika tutaweka wazi kila kitu, lakini mie naangalia wachezaji wenye uwezo na watakaofaa kuungana na timu yangu" alisema Msimu.

Aliongeza kuwa kwa sasa wachezaji wao wamepewa likizo na wanatarajia kuanza mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya baada ya kumalizika kwa kipindi cha Ramadhani.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 36 | 29 | 4 | 3 | 76 | 14 | 91 |
| 2. Yanga | 37 | 27 | 5 | 5 | 57 | 25 | 86 |
| 3. Azam | 37 | 20 | 12 | 5 | 52 | 21 | 72 |
| 4. Kinondoni MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5. Mtibwa Sugar | 37 | 14 | 7 | 16 | 36 | 34 | 49 |
| 6. Lipuli | 37 | 12 | 13 | 11 | 31 | 37 | 49 |
| 7. Mbeya City | 37 | 13 | 8 | 16 | 38 | 40 | 47 |
| 8. Ndanda | 37 | 12 | 12 | 13 | 24 | 34 | 48 |
| 9. Singida United | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 10. Stand United | 36 | 12 | 8 | 16 | 36 | 45 | 44 |
| 11. Alliance | 36 | 11 | 11 | 14 | 30 | 39 | 44 |
| 12. Coastal Union | 36 | 10 | 14 | 12 | 31 | 42 | 44 |
| 13. Mbao | 37 | 11 | 11 | 16 | 26 | 40 | 44 |
| 14. TZ Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 15. Biashara United | 36 | 11 | 10 | 15 | 29 | 34 | 43 |
| 16. Kagera Sugar | 36 | 10 | 13 | 13 | 32 | 40 | 43 |
| 17. Ruvu Shooting | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 18. Mwadui | 37 | 10 | 8 | 18 | 44 | 53 | 41 |
| 19. KT Tanzania | 36 | 9 | 14 | 13 | 24 | 34 | 41 |
| 20. African Lyon | 37 | 4 | 11 | 22 | 23 | 51 | 23 |

# MAKAMBO AFUNGUKA JINSI ATAKAVYOPAMBANA HOROYA

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Heritier Makambo, amesema kuwa amejiandaa kwenda kupambana na changamoto mpya katika klabu yake mpya ya Horoya AC ya Guinea.

**Makambo ambaye ameitumikia Yanga kwa msimu mmoja, amesaini mkataba wa miaka mitatu na klabu hiyo ya Guinea huku viongozi wa Yanga wakisema kuwa bado ni mchezaji wao halali.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Makambo, alisema kuwa ameshakamilisha mchakato wa kujiunga na klabu hiyo na sasa kilichobakia ni kumalizia mechi moja ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambayo Yanga itacheza dhidi ya Azam FC.

Makambo alisema kuwa anaondoka Yanga, lakini hatasahau wachezaji, viongozi pamoja na kocha wake Mwinyi Zahera ambao kwa muda wote waliishi kama familia moja.

"Mambo yangu yote na Horoya yameshamalizika, nasubiri ligi imalizike halafu nikakumbane na changamoto mpya, nitakumbuka vitu vingi vya Yanga, lakini zaidi sitamsahau Chicharito (Godlisten Anderson- Ofisa Habari Msaidizi wa Yanga), mtu wa karibu yangu, tunapambana naye sana," alisema Makambo.

Mshambuliaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema kuwa haikuwa kazi rahisi kukamilisha mchakato huo wa kujiunga na Horoya, lakini anamshukuru Mungu usajili wake umekamilika.

Makambo ameisaidia Yanga kumaliza katika nafasi ya mbili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa amefunga mabao 17 wakati kinara wa kupachika magoli ni mshambuliaji wa Simba Mnyarwanda Meddie Kagere aliyezitingisha nyavu za wapinzani wao mara 23.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisisitiza kuwa Makambo ni mchezaji wa Yanga ambaye mkataba wake utamalizika Juni mwakani.

Mwakalebela alisema kuwa taarifa za Makambo kusajiliwa Yanga kwa mkopo akitokea FC Lupopo si za kweli na zimetengenezwa na watu wasioitakiwa mema klabu hiyo.



Mtaalamu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Agness Gidna (kulia), akitoa maelekezo juu ya historia ya chimbuko la mwanadamu kwa wachezaji na viongozi wa Sevilla FC kutoka Hispania walipotembelea katika kituo hicho jana asubuhi. Sevilla FC imekuja nchini kwa udhamini wa Kampuni ya Sportpesa Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Serikali yaitaka TFF kubadilika*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imelitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuacha kufanya kazi zake kwa upendeleo ili kuharakisha maendeleo ya mchezo huo.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na serikali za mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo wakati akifunga semina ya Maafisa Michezo nchini iliyokuwa inafanyika jijini hapa.

Waziri Jafo alisema hakuna sababu ya shirikisho hilo kuendekeza "majungu" kwa maslahi yao wenyewe, na kama wataendelea na mfumo huo watakuwa wanashiriki kuua soka la nchi.

Jafo alisema endapo kutakuwa na vitendo vya upendeleo, jambo hilo litakatisha tamaa wachezaji wa timu nyingine licha ya kuwa na uwezo wa kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

Waziri huyo alisema kuwa timu za hapa nchini zinafanya vema katika mechi zake mbalimbali licha ya kukabiliwa na tatizo la ukata lakini zimekuwa zikijitahidi kupambana hadi katika michezo yake ya mwisho ya msimu.

Aliipongeza Yanga iliyokuwa inachuana na klabu "tajiri" (hakuzitaja)kwa kushika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu licha ya kuwa na matatizo ya fedha.

"Yanga ilikuwa kama mtoto yatima mwenye njaa lakini akiingia darasani anafanya vizuri, Yanga imesumbua sana kwenye ligi na inastahili pongezi kwa sababu imepambana na watoto wanaokula mkate kwa blueband," alisema Jafo.

Aliwataka TFF kujitathmini na kuacha kufanya kazi bila ya kufuata kanuni na taratibu na kuweka mbele maslahi ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Michezo

Ijumaa Mei 24, 2019

Nipashe




Deschamps: Nipo tayari kumpeleka Pogba Real UKURASA 28




# ZAHERA AMPA AJIBU 'NONDO'

## Ni baada ya kusajiliwa na TP Mazembe...

**Na Somoe Ng'itu**

IKIWA ni siku chache zimepita tangu nahodha na mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu, asajiliwe na timu ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kocha wake, Mwinyi Zahera, amemtaka nyota huyo ajipange kwenda kupambana ili aweze kupata namba kwenye kikosi hicho cha mabingwa wa zamani wa Afrika.

**Ajibu ni mchezaji wa pili wa Yanga kuondoka ndani ya wiki moja baada ya mshambuliaji Mkongomani Heritier Makambo kusajiliwa na Horoya AC ya Guinea.**

Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam, Zahera, alisema kuwa amefurahishwa na usajili huo lakini akasisitiza kwamba mshambuliaji huyo anatakiwa kubadilika ili aweze kudumu katika kikosi hicho cha TP Mazembe.

"Ajibu ni mchezaji mzuri, lakini anatakiwa kujituma sana ili aweze kucheza, TP Mazembe ni kubwa sana, kama atalala hawezi kupata nafasi ya kucheza, ana akili ya mpira, " alisema Zahera.

Kocha huyo alisema kuwa Ajibu atakwenda kukutana na mfumo mpya ambao utamhitaji kuonyesha bidii wakati wote na kueleza kwamba huko hakuna mwandishi ambaye anamwandika.

"Kule hakuna gazeti ambalo litakuwa linamwandika, hali hiyo itamfanya ajitume ili kupandisha kiwango chake, itakuwa vizuri kwake, ataona kama sio Ajibu peke yake na yeye huko si mchezaji nyota pekee, kuna 'staa' wengi," Zahera alisema.

Alieleza kuwa Yanga ilianza kufanya mawasiliano na TP Mazembe tangu wiki tatu zilizopita na sasa hatimaye wamefanikiwa kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji huyo wa zamani wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini.

Aliongeza kuwa kuondoka kwa Ajibu hakutakuwa pengo katika kikosi cha Yanga kwa sababu anaamini benchi lake la ufundi litafanikisha kusajili mshambuliaji mwingine atakayeziba nafasi hiyo na hatimaye Yanga kurejea kwenye ushindani katika msimu ujao.

"Ni kweli anakwenda, TP Mazembe walizungumza na mimi tangu wiki tatu zilizopita, kwa kuondoka Ajibu, atakuja Ajibu mwingine," alimaliza kocha huyo ambaye anafanya kazi pamoja na kocha wa TP Mazembe, Florent Ibenge katika kikosi cha Timu ya Taifa ya DRC.

Ajibu anajiunga na TP Mazembe kama mchezaji huyo baada ya mkataba wake na Yanga kubakiza siku chake wakati klabu hiyo pia ikionekana huenda ikaambulia patupu kwenye usajili wa Makambo.

# Hatima Niyonzima Simba hadharani

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa kimataifa wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, Haruna Niyonzima, amesema kuwa anaamini mazungumzo yake na mabosi wa klabu hiyo yatamalizika vema.

Niyonzima (pichani chini) ambaye ametwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara mara mbili mfululizo akiwa na Simba, alijiunga na mabingwa hao mwaka juzi akitokea kwa watani zao Yanga ambako pia aliwatumikia kwa mafanikio.

Akizungumza na Nipashe, Niyonzima, alisema kuwa mchakato wa mazungumzo ya kusaini mkataba mpya ulishaanza na sasa kila upande unajiridhisha kwa kuzingatia maslahi na malengo ya msimu ujao.

"Kwa sasa hivi siwezi kuweka kila kitu wazi, muda utakapofika taarifa zitawekwa hadharani, ngoja tumalizie msimu huu kwanza," alisema kiungo huyo wa zamani wa APR ya Rwanda.

Alisema kuwa anaamini juhudi zake za kujituma na kutokata tamaa zimechangia kupata mafanikio licha ya baadhi ya wadau kumwona ni mchezaji ambaye hataisaidia Simba.

"Nilianza vibaya kutokana nilikuwa majeruhi, siri ya mafanikio yangu nilikuwa na subira, na baada ya kutoka katika maumivu nilipambana, sikusikiliza watu, watu waliongea mengi," alisema Niyonzima baba wa watoto watatu.

Tangu alipowasili Tanzania, Niyonzima ametwaa mataji matano ya Ligi Kuu Tanzania Bara, matatu akiwa na Yanga na mawili akiwa na kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >